BARAZA LA HABARI TANZANIA

KANUNI ZA MAADILI KWA WANATAALUMA WA HABARI

Toleo la 2016

KANUNI ZA MAADILI KWA WANATAALUMA WA HABARI

© Media Council of Tanzania, 2016

ISBN 978-9987-710-59-1

YALIYOMO

DIBAJI 1

MAANA YA DHANA NA MANENO MUHIMU 3

Kanuni za Maadili Kwa Wakuu wa Vyombo vya Habari/Wahariri

1.0 Wakuu wa Vyombo vya Habari/Wahariri 6
1.1 Migongano ya Maslahi 6
1.2 Shinikizo au Ushawishi 6
1.3 Ushabiki 6
1.4 Ushindani wa Taaluma 7
1.5 Mishahara na marupurupu 7
1.6 Kupambana na Rushwa 7
1.7 Kanuni/Viwango vya Uhariri 8
1.10 Utaratibu wa Mrejesho 13
1.11 Ubaguzi 13
1.12. Ghiliba 13
1.13 Uhalifu na Tabia Mbaya 13
1.14 Kashfa na maudhui yake 14
1.15 Masuala Yanayohusiana na Dini 14
1.16 Uwajibikaji na Wajibu 14
1.17 Maudhui ya habari za mtandaoni 15

Kanuni za Maadili kwa Afisa Uhusiano/Afisa Mawasiliano

2.0 Afisa Uhusiano/Afisa Mawasiliano 16
2.2 Haki 16
2.3 Utetezi/Ukuzaji 16
2.4 Utiifu/Uaminifu 16
2.5 Maelewano 17
2.6 Tunu za Taifa 17
2.7 Uwajibikaji na wajibu 17
2.8 Maudhui ya habari za mtandaoni 17

Kanuni za Maadili kwa Mawakala wa Matangazo wa Vyombo vya Habari

3.0 Mawakala wa matangazo wa vyombo vya habari 19
3.1 Ukweli 19
3.2 Lugha 19
3.3 Uthibitisho 19
3.4 Vionjo na Heshima 20

3.5 Madai 20
3.6 Tunu za taifa 20
3.7 Kashfa 20
3.8 Ubaguzi 20
3.9 Watoto 20
Maudhui 20
Usalama 21
3.10 Vileo, Tumbaku, Usalama Barabarani na Mazingira 21
3.11 Uwasilishi 21
3.12 Mashindano 22
3.12 Matangazo ya Utata na Kisiasa 22
3.13 Udhamini 22
3.14 Kanuni za Maadili 22
3.15 Tangazo la Ushuhuda 22
3.16 Uwajibikaji na wajibu 23
3.17 Maudhui ya habari za mtandaoni 23

Kanuni za Maadili kwa Watangazaji

4.0 Watangazaji 24
4.1 Kanuni za Maadili 24
4.2 Viini vya tunu 25
4.3 Vionjo na Heshima 26
4.4 Maelezo Hatari au Tabia Mbaya 27
4.5 Unyeti wa Jinsia 28
4.6 Uhalifu na Vurugu 28
4.7 Machafuko na huzuni 28
4.7 Onyo na Kuvuruga au Uvunjivu wa Maudhui 29
4.8 Kashfa 29
4.9 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Utendaji wa Wahariri 29
4 .10 Matangazo ya Kutangazwa: 31
Maudhui 32
Usalama 32
4.11 Uchambuzi, Maoni na Tahariri 34
4 .12 Habari zinazohusisha watoto 35
4.13 Haki ya kujibu 36
4.14 Faragha 36

4.15 Vipindi vya moja kwa moja vya Simu 37
4.16 Hali ya Usimamizi na Heshima 37
4.17 Masuala yanayohusiana na Imani 37
4. 18 Kuepuka Uragbishi 38
4.19 Viwango vya Kuhariri na Kutayarisha vipindi 38
4.20 Haki za kunakili 38
4.21 Wizi wa Maandishi na Mawazo 38
4.22 Maudhui ya Mtandaoni 39

Kanuni za Maadili kwa Wapiga picha wa magazeti na Wasimamizi wa Video

Msimamizi wa Video: 40

5.1 Kanuni za Maadili 40
5.2 Tunu muhimu 41
5.3 Uadilifu wa taaluma 42
5.4 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Uhariri 42
5.5 Vitendo vya kupiga vita rushwa 46
5.5 Kuingia mahali bila kuruhusiwa 47
6.13 Maudhui ya habari za mtandaoni 47

Kanuni za Maadili kwa Waandishi wa Habari

6.0 Waandishi wa Habari 49
6.1 Kanuni za Maadili 49
6.2 Kanuni za tunu 50
6.3 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Uhariri 52
6.10 Maslahi binafsi na Ushawishi 56
6.5 Vitendo vya kupiga vita rushwa 56
6.6 Mahusiano yasiyo na Hatia 57
6.7 Masuala Yanayohusiana na Imani 57
6.8 Huzuni 58
6.9) Vitendo vya kupiga vita rushwa 58
6.10 Uhuru wa Vyombo vya Habari na Wajibu wa Jamii 59
6.11 Ghiliba 59
6.12 Uchochezi 59
6.13 Maudhui ya mtandaoni 59

Miongozo kwa Wamiliki wa Vyombo vya Habari na Wachapishaji

7.0 Wamiliki wa Vyombo vya Habari/Wachapishaji 61
7.0 Uhuru 61

7.1 Ushindani 61
7.2 Shinikizo au Ushawishi 61
7.3 Malipo ya Habari na Mauzo 61
7.4 Uchunguzi 62
7.5 Migongano ya Maslahi 62
7.6 Shinikizo au ushawishi 62
7.7 Ushabiki 62
7.8 Uwezo Kitaaluma 63
7.9 Mishahara na Marupuru 63
7.10 Shuruti na Vitisho 63
7.11 Uwajibikaji kwa jamii 63
7.12 Wajibu na Uwajibika 64
7.13 Kushughulikia maudhui mapya ya vyombo vya habari 64
MAREJEO 64

DIBAJI

Maadili ni kanuni za jumla zilizokubaliwa kuwekwa na wadau wa habari, ili kutoa taratibu za misingi ya viwango vya taaluma ya tasnia ya habari. Kanuni hizo zinalenga kutawala mienendo na tabia au vitendo vya wanataaluma wa habari katika utendaji wa majukumu yao.

Kanuni za maadili, ambazo kwa kawaida ziko katika nyaraka, hutumika kama mwongozo wa hadidu rejea kwa wanataaluma wa habari wakati wanapochukua maamuzi makini kuhusu changamoto za taaluma na maadili katika shughuli zao za kila siku za kukusanya, kutengeneza na kusambaza habari. Kanuni hizo zina maana ya kuwaongoza wanahabari wakati wanapofanya tathmini makini ya shughuli zao za kila siku kama wanamawasiliano na wapashaji habari.

Sababu halisi ya kuwa na kanuni za maadili ni kuhakikisha wanahabari wanakuwa na hadidu rejea zinazowaongoza na kuwasaidia kuzingatia viwango vya juu vinavyohitajika kulingana na majukumu yao ya uwajibikaji kitaaluma kwa jamii. Kwa upande mwingine, kanuni inawaelekeza wanataaluma wa habari kazi na majukumu yao katika jamii wanayoihudumia.

Baraza la Habari Tanzania (MCT), chombo kinachojitegemea na kinachojiendesha chenyewe hushughulikia sheria za mienendo ya vyombo vya habari nchini na kwa kutambua umuhimu wa kanuni za maadili kwa wanataaluma wa habari , kimeshirikiana na wadau wengine wa habari kutengeneza kijitabu hiki ili kitumike kama muongozo wa hadidu rejea kwa wanahabari hapa nchini. Baraza linaamini kwamba ni kwa kuendesha shughuli ndani ya viwango vya maadili, uhuru wa vyombo vya habari unaokuzwa na baraza ndiyo utanufaisha jamii.

Wafuatao ndiyo walengwa wa kanuni hizi za maadili: wamiliki wa vyombo vya habari na wachapishaji, maofisa uhusiano na watoa matangazo katika vyombo vya habari na muhimu zaidi ni wanahabari wote wa ndani na nje wanaofanya kazi katika Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Hao ni pamoja na wakuu wa vyombo vya habari, wahariri, maafisa uhusiano, mawakala wa matangazo wa vyombo vya habari, watangazaji, wapigapicha, wasimamizi wa vipindi vya video, waandishi wa habari binafsi, waandishi wa makala, wachoraji wa vibonzo pamoja na wamiliki wa vyombo vya habari na wachapishaji. Kanuni hizi za maadili pia zinawabana watoa habari kwa njia ya mitandao.

Kanuni hizi za maadili kwa wanahabari zina sehemu saba za majukumu ya wakuu wa vyombo vya habari na wahariri, maafisa uhusiano na mawasiliano, mawakala wa matangazo wa vyombo vya habari, watangazaji, wapigapicha na wasimamizi wa video, waandishi wa habari pamoja na wamiliki wa vyombo vya habari na wachapishaji.

MAANA YA DHANA NA MANENO MUHIMU

Wanahabari: Wanahabari ni watu waliopata mafunzo ya uandishi wa habari na wanafanya shughuli za habari na mawasiliano

Maslahi ya Umma: Maana ya maslahi ya umma yanatumika katika aina nyingi kulingana na muktadha unaohusika. Kwa muktadha wa kanuni hizi za maadili , maslahi ya ya umma yanagusa yafuatayo: masuala yote ya faida kwa watu wote wa kawaida, masuala ambayo kwa jumla yanagusa umma, masuala ambayo yanatambua, kulinda na kuendeleza ustawi wa umma kwa jumla.

Uchochezi: Ni uchochezi wa kutia chumvi katika matukio na mambo mengine katika habari. Hiyo ni pamoja na kuandika mambo madogo na ya upendeleo yaonekana makubwa kupita kiasi. Kutia chumvi pia kunahusu kuandika kwa makusudi habari ambayo kwa namna fulani italeta wasiwasi na hisia kubwa kwa wasomaji au wasikilizaji.

Ushabiki: Kuandika habari kuhusu kitu kisichokuwepo kabisa. Hiyo ni pamoja na kufuata na kuamini kitu bila kuhoji. Ushabiki hujionyesha wenyewe kwa mapenzi kama ya dini, makundi maalum ya kisiasa, mila za kikabila, na hali halisi ya ushabiki unaojitokeza kama katika klabu za michezo. Kwa upande wa uandishi wa habari, ushabiki hufanywa kuunga mkono makundi katika jamii kwa kitu kisichokuwepo. Hiyo inaathiri uwezo wa maamuzi ya mwandishi anaposhughulikia habari.

Vijembe/kashfa: Kutumika maelezo yasiyokuwa ya moja kwa moja kuhusu mtu fulani au kitu. Kwa kawaida ni hali ya kuumbua au kushusha hadhi ya mtu. vijembe hutokea wakati maneno yanapotolewa wasomaji au watazamaji wanaweza kumtambua mtu anayelengwa. Kwenye mahakama na Baraza la Habari aina hiyo ya habari inaweza kutafsiriwa kuwa ni kushusha hadhi ya mtu hata kama mtu mwenyewe aliyelengwa hakuwa huyo, ili mradi idadi ya wasomaji au watazamiaji wanaweza kutoa ushahidi

wa kuamini maneno yalihusu mtu huyo.

Ubaguzi: Kubandikiwa sifa kwa makundi ya watu kutokana na rangi yao, utaifa, muonekano wa kijinsia na kusababisha ubaguzi na kupuuza watu tofauti ndani ya makundi.

Hotuba ya chuki: Inahusu shambulio kwa mtu au kundi kwa misingi ya rangi, dini, jinsia na muonekano ukiwemo wa kimwili au utaifa na kuwa na uwezo wa kuchochea chuki, kutoelewana na vurugu. Hotuba ya chuki vile vile ni mawasiliano yanayokusudia kushusha hadhi ya mtu, kuzuia au kuchochea vurugu au kuchukua hatua ya upendeleo kwa mtu mwingine kwa misingi ya rangi, ukabila, asili ya utaifa, dini, muonekano wa kijinsia au aina yoyote ile ya ulemavu.

Vitendo vya rushwa: Ushawishi wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, au kuomba kupata upendeleo kutoka kwa watu walioko katika nafasi zao au vinginevyo kushawishi baadhi ya matokeo.

Migongano ya Maslahi: Uwezo wa kukwamisha uadilifu wa mtu kwa sababu ya uwezekano wa kutokea mgongano kati ya maslahi binafsi ya mtu na maslahi ya taaluma au umma. Kwa maneno mengine, mgongano wa maslahi ni hali ambayo uwajibikaji wa upande mmoja kwa mwingine kunazuia kutimiza wajibu.

Uhuru wa Vyombo vya habari: Unahusu uwezo wa chombo kutumia habari iliyopokelewa bila hofu ya kuadhibiwa. Pia inahusu chombo cha habari kisichodhibitiwa na kikundi chochote chenye maslahi, lakini bado kina fursa ya kupata habari muhimu.

Uwajibikaji: Kuchukua kikamilifu jukumu la matokeo ya vitendo au shughuli zinazofanywa na mtu mwingine au kuyachukulia matokeo hayo kwa moyo, hiari na kuchukua kwa weledi maamuzi yake yanayohusika.

Uwajibikaji kwa jamii: Haya ni majukumu yanayoelekeza vyombo vya habari kuweka msisitizo zaidi katika kukuza ustawi wa jamii badala maslahi ya kibiashara tu.

Wizi wa maandishi/mawazo: Kitendo cha kutumia maandishi na mawazo ya mtu mwingine bila ya kibali chake au kutaja chanzo chake.

Vionjo: Vionjo vina uhalisia tofauti kutoka sehemu moja hadi nyingine katika jamii hadi nyingine na hivyo kuwa vigumu kwa watangazaji kuweka viwango vya vionjo vinavyokubalika na jamii ya watu wote.

Heshima: Inahusu kuheshimu misingi ya desturi na mila za watu wote na imani zao. Pia huonekana tofauti kutegemeana na taswira ya mtu.

Maudhui ya mtandaoni: Kinachozungumziwa hapa ni utayarishaji wa habari kwa njia ya teknolojia mpya za mawasiliano (tofauti na vyombo vya kawaida vya habari yakiwemo magazeti, TV au Luninga na Radio). Hiyo ni pamoja na mtandao, tovuti, multimedia, CD-ROM na DVD.

Kanuni za Maadili Kwa Wakuu wa Vyombo vya Habari/Wahariri

1.0 Wakuu wa Vyombo vya Habari/Wahariri

Hawa ni watu wanaohusika na uchaguzi na utayarishaji wa habari za runinga, redio na magazeti ili kutoa taarifa au habari kwa wasomaji, watazamaji na wasikilizaji. Kwa hiyo miongoni mwa kazi zao ni kuhariri habari. Wakuu wa Vyombo vya habari na wahariri wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1.1 Migongano ya Maslahi

i) Hawana budi kuwa huru kwa jumuiya na kuepuka shughuli zinazoweza kushawishi maamuzi ya kitaaluma, kuhatarisha uadilifu wao na kuharibu sifa ya taaluma.

ii) Wanataaluma waachwe wafanye maamuzi ya mwisho kuhusiana na kazi ya uhariri. Kwa njia zote zile, kazi ya uhariri ni lazima izingatie matakwa ya wasomaji, watazamaji na wasikilizaji kulingana na maoni ya wahariri.

1.2 Shinikizo au Ushawishi

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wawe huru katika majukumu yao mbali na haki ya umma kupata habari na kufahamu mambo yanayotokea ndani na nje ya nchi pamoja ustawi wa jamii. Kwa maneno mengine, hawatabinya wala kupotosha habari ambayo umma una haki ya kufahamu au kujua kwa sababu tu ya shinikizo la ushawishi wa maslahi ya kisiasa, kibiashara au kijamii.

1.3 Ushabiki

Wakuu wa Vyombo vya Habari na Wahariri wasijihusishe na aina yoyote ya ushabiki unaoweza

kuathiri uadilifu wao katika kutendea haki habari kwa kutoegemea upande wowote.

1.4 Ushindani wa Taaluma

Kuna umuhimu wakuu wa vyombo vya habari na wahariri kuhimiza wafanyakazi kuboresha uwezo wa utendaji wa ushindani kupitia mafunzo na kujiendeleza kielimu. Zaidi ya hapo hawana budi kuhakikisha watumishi wao wanapata ubunifu mpya katika tasnia ya mawasiliano.

1.5 Mishahara na marupurupu

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wahimize wamiliki wa vyombo vyao vya habari kuwalipa wafanyakazi kwa mujibu wa sifa za taaluma na utendaji wao wa kazi.

Katika vyombo vyote vya habari hapana budi kuwepo mpango wa utumishi unaoelezea wazi masuala yanayohusiana mbali na mashahara, marupurupu na motisha.

1.6 Kupambana na Rushwa

i) Zawadi na Takrima

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wakatae tuzo, burudani, zawadi au upendeleo wa aina yoyote ile unaoweza kwa njia yoyote ile kushawishi au kuonekana kushawishi maamuzi yao ya kitaaluma. Katika mahali ambapo zawadi zinatolewa, mpokeaji ni lazima aeleze na kuwafahamisha wakuu wake wa kazi kuhusu upokeaji wa zawadi hiyo au kitu kingine alichotendewa.

ii) Fadhila

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wasikubali kupokea kitu chochote cha upendeleo

ili kuepuka kufika mahali ambapo watahitajika kulipa fadhila hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao. Vivyo hivyo, wasitumie nafasi zao au fursa waliyopata kutokana na nafasi zao kwa faida binafsi.

iii) Malipo ya Habari /Vyanzo

Wakuu wa vyombo vya habari na Wahariri wasitoe fedha au zawadi kushawishi vyanzo kutoa habari kwani kufanya hivyo ni sawa na kugeuza habari iwe aina ya bidhaa kibiashara, kitu ambacho hakitakiwi kiwe hivyo.

iv.) Kupokea Malipo ya Kutoa Habari

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wasipokee fedha au aina yoyote ya malipo kama kichocheo cha kuchapisha au kutangaza habari.

1.7 Kanuni/Viwango vya Uhariri

i) Uhariri

Kanuni zitahakikisha maudhui yaliyochapishwa au kutangazwa yanakidhi viwango vya ubora na taaluma, hakuna nia mbaya ya uvunjifu au kashfa katika uhariri ambao unatakiwa ulingane na sera na kanuni za chombo husika cha habari na kwa mujibu wa sheria za nchi.

ii) Wajibu na Uwajibikaji

Wahariri watawajibika kwa habari zote zilizochapishwa au kutangazwa katika chombo cha habari na matokeo mengine ya maudhui ya habari hizo.

iii) Ukweli na Uhakika

Wahariri watofautishe kabisa kati ya ukweli na uhakika, ubahatishaji wa kitu, maoni na mawazo.

iv) Hatia

Katika uandishi wa habari wahariri wazingatie

kanuni kwamba mtu yeyote anayeshtakiwa au kushukiwa kufanya kosa anapaswa kuchukuliwa kuwa hana kosa hadi ithibitishwe mahakamani ana hatia mbele ya sheria.

v) Faragha

Wahariri wazingatie faragha ya kitaaluma kuhusu chanzo cha habari inayopatikanna kwa siri. Wana wajibu wa kukilinda chanzo cha habari cha siri isipokuwa wanapolazimizika kuvitaja kwa amri ya mahakama.

vi) Habari iliyotolewa kwa mwandisshi kwa taarifa yake tu.

Wakuu wa Vyombo vya habari/wahariri waheshimu ahadi ya kuacha kutumia baadhi ya habari kwa kuchapisha au kutangaza iwapo waandishi walikiahidi chanzo kwamba habari hiyo ilikuwa ni kwa ufahamisho wao tu na haitatumika.

vii) Usahihi na Masahihisho

a) Hakikisha vyombo vya habari, wakati wote, vinaongozwa na usahihi wa habari na havipotoshi kwa makusudi au kuwaarifu isivyo wasomaji, watazamaji au wasikilizaji. Hakikisha habari inayochapishwa au kutangazwa ni sahihi na kuweka mizania ya pande zote zinazohusika.

b) Hakikisha machapisho hayajiingizi kwenye maoni yasiyokuwa na haki, yenye udanganyifu, upotoshaji au utoaji mbaya wa ukweli.

c). Machapisho yasipotoshe kwa makusudi au kuwaarifu isivyo wasomaji, watazamaji au wasikilizaji kwa kuweka au kuacha kitu kilichokusudiwa. Hakikisha hakuna vitu visivyo na msingi, vinavyopotosha au

kukosa ukweli.

d). Wakati wowote inapobainika au kugundulika kuwa habari iliyochapishwa au kutangazwa siyo sahihi, inapotosha au imevurugwa, ni lazima isahihishwe mara moja mapema kabla ya kuanza kutokea malalamiko.

e) Hakikisha masahihisho ni dhahiri na pande ziliazoathirika kuombwa radhi. Kwa minajili ya uwazi na usahihi, makosa yaliyojitokeza na mapungufu yapewe ufafanuzi kuhusu habari iliyopotoshwa au kuvurugwa.

f) Hakikisha vichwa vikuu vya habari, vichwa vidogo na maelezo ya picha yanabeba na kuwasilisha maudhui halisi ya taarifa husika.

g) Gazeti lihakikishe picha au sura zilizobadilishwa kitaalamu zisichapishwe kwanza bila ya kuwaarifu wasomaji ukweli halisi na ikibidi, sababu na umuhimu wa kufanya hivyo ziandikwe. Katika kuepuka kuibua hisia mbaya kwa wahusika, picha zinazohusu matukio ya huzuni na mshituko zitumiwe kwa uangalifu.

viii) Haki ya kujibu

a) Yanapokuwepo malalamiko kutoka kwa watu binafsi, makundi au taasisi kutokana na makosa yaliyotokea katika habari iliyochapishwa au kutangazwa, fursa ya haki itendeke kuwajibu wahusika. Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri bila kuchelewa na kwa heshima, wachapishe au kutangaza masahihisho ya makosa yaliyofanyika katika habari iliyochapishwa

au kutangazwa katika vyombo vyao vya habari.

b). Pale mhariri anapokuwa na ushahidi wa kutosha pasipo mashaka na uhalisia wa ukweli na usahihi wa jibu au ufafanuzi wake, atakuwa huru kuongeza kama sehemu tofauti mwishoni mwa ufafanuzi wake kwa kutoa maelezo mafupi kuonyesha msimamo wake kuhusiana na suala hilo.

ix) Faragha

a) Uchapishaji bila kibali wa habari na picha kuhusu maisha ya faragha ya watu au maslahi yao unaruhusiwa, iwapo tu ni muhimu kwa wananchi kujua ukweli na pia kama kwa maslahi ya taifa uhalali wake unazidi haki ya faragha ya wahusika.

b) Aidha kuchapisha bila idhini habari kama hizo au kuchunguza maisha ya faragha au maslahi ya watu binafsi inaruhusiwa iwapo tu habari husika ni lazima ichapishwe kwa manufaa ya umma na kwa kufanya hivyo mhariri haingilii uhuru na haki ya faragha ya mhusika.

c) Ifahamike 'Manufaa ya umma' hayahusiana kwa karibu na'shauku ya wananchi kutaka kujua kitu.' Kwani kuwa mashuhuri katika jamii hakuondoi haki ya mtu kuwa huru katika maisha yake ya faragha isipokuwa tu kama hali hiyo inaathiri utendaji wake binafsi kwa mujibu wa nafasi yake katika jamii.

d) Hapa maslahi ya umma yanayojitokeza zaidi kama ilivyo kwenye vifungu vingine vya kanuni za maadili ni pamoja na:upelelezi au kufichua uhalifu; kulinda afya na

usalama wa raia na kuzuia raia wasipotoshwe vibaya na mtu au taasisi katika mambo muhimu yanayowahusu.

xi) Masuala ya Kutisha na Machungu katika Jamii

Kulingana na wajibu wake wa kuchapisha au kutangaza habari za maslahi ya umma kulingana na umuhimu wake, vyombo vya habari katika kushughulikia masuala ya jamii hasa yenye hisia ya kutisha na machungu makali kama maovu, vurugu, matumizi ya dawa za kulevya, ukatili, utesaji, udhalilishaji wa kijinsia na uchafu mwingine, umakini maalum unahitajika wa namna ya kuwasilisha ukweli, maoni, picha au michoro kwa uangalifu unaostahili.

xii) Wizi wa maandishi/mawazo

a) Wakati wote epuka kujihusisha na wizi wa maandishi na mawazo. Hiki ni kitendo cha kutumia maandishi na mawazo ya mtu mwingine bila ya kibali chake au kutaja chanzo chake.

b) Maneno yanayokaririwa moja kwa moja kutoka kwenye vyanzo vingine mbali na yale yaliyoandikwa na mwandishi mwenyewe hayana budi kutajwa chanzo chake. Kwa jumla, kazi nyingine inapotumika kama chanzo cha mawazo ni lazima kazi ya mwisho itofautiane na kazi halisi ili kukidhi aina na mtindo wa uandishi wa kazi ya mwisho.

c) Uwajibikaji wa kazi ya mwisho utakuwa wa mhariri ili kuhakikisha yaliyochapishwa au kutangazwa hayana wizi wa mawazo, maandishi au kazi kutoka vyanzo vingine na kama vipo ni muhimu kuwataja ipasavyo wahusika.

1.10 Utaratibu wa Mrejesho

i) Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wanawajibika kubeba na kushughulikia madai/ lawama zote zinatolewa na wasomaji, watazamaji na wasikilizaji. ii)Machapisho au vituo lazima viweke utaratibu ambao utawezesha umma kushiriki kikamilifu katika utoaji taarifa, habari na mawazo.

1.11 Ubaguzi

Wahariri wahakikishe habari zisiwe na ubaguzi wa jinsia, dini, makundi ya watu wachache, hadhi ya jamii, masuala ya ngono, umri, kabila, rangi, au ulemavu wa aina yoyote ile. Hata hivyo, pale inapokua muhimu kwa manufaa ya umma, habari hiyo iwe na maoni ya watu.

1.12. Ghiliba

Hakikisha waandishi wa habari na wapiga picha wanatumia njia za moja kwa moja kupata habari au picha, kwa kawaidakwa kujitambulisha wenyewe wanapofanya hivyo. Utumiaji wa ghiliba kupata habari au picha unaweza kuhalalishwa tu katika mazingira yasiyo ya kawaida wakati kitu kinachotafutwa kwa maslahi ya umma hakipatikani kwa njia nyingine yoyote. Matumizi ya ghilba lazima yaelezwe kama sehemu ya stori.

1.13 Uhalifu na Tabia Mbaya

i) Hakikisha waandishi hawatukuzi uhalifu na tabia mbaya katika jamii, hasa kwa kuhusisha vurugu au ukatili. Wasiandike, kuonyesha au kutoa maelezo zaidi ya uhalifu kwa namna ambayo inaweza kushawishi au kuchochea watu kuiga au kufanya majaribio ya matukio hayo. Wahariri hawana budi kujua na kuelewa mambo hasa

yaliyomo katika habari, na uwezekano wa athari zake kwa wasomaji, watazamaji na wasikilizaji.

ii) Kwa sababu hiyo habari ya aina hiyo isichapishwe au kutangazwa, isipokuwa tu kama imeruhusiwa kisheria na hivyo kwa manufaa ya umma wasitajwe waathirika wa uhalifu na udhalilishaji wa ngono; wala kijana anayeshtakiwa kwa kosa la uhalifu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 na ambaye huko nyuma hajawi kutiwa hatiani na kuwatambulisha bila ridhaa ndugu wa mtu anayeshtakiwa au kutiwa hatiani kutokana na kosa la uhalifu.

1.14 Kashfa na maudhui yake

Habari au tangazo lenye taarifa inayoweza kuwa ya kashfa, au yenye kuelekea kuwa na nia mbaya, isichapishwe. Pale ambapo habari ya namna hiyo ni lazima ichapishwe au kutangazwa, basi uamuzi wake ni lazima usichukuliwe na mhariri peke yake. Badala yake ijadiliwe na wahariri wandamizi na kama lazima upatikane ushauri wa wakili au mshauri yoyote wa mambo ya kisheria.

1.15 Masuala Yanayohusiana na Dini

Katika kuleta usawa, haki na namna bora katika kuzingatia masuala ya dini, wanahabari wazungumze na viongozi wa dini kwa kutambua heshima na staha yao na jinsi imani zao zinavyofuatwa na wafuasi wao.

1.16 Uwajibikaji na Wajibu

i) Wahariri watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kuwa kipaumbele chao badala ya shughuli zao za kawaida, maslahi na uhuru binafsi.

ii) Watahesabu habari kama bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa. Vivyo hivyo watawajibika siyo

kwa wale wanaothibiti au kumiliki vyombo vyao vya habari bali kwa umma na kwa sehemu kubwa yakiwemo maslahi ya jamii.

iii) Watawajibika kutokana na matokeo yatokanayo na vitendo vya taaluma yao au vitendo vilivyofanywa au kuchukuliwa kwa moyo, hiari na kufanya maamuzi kwa weledi. Chini ya mazingira hayo yote hatua ichukuliwe kulingana na ufahamu wa maadili.

1.17 Maudhui ya habari za mtandaoni

i) Kwa maudhui ya habari zinazowekwa kwenye mtandao, wakuu wa vyombo vya habari na wahariri watabidi wawe makini kwa kuangalia mara kwa makini ili kujiridhisha pasipo mashaka kuhusu maudhui yake ili kuhakiki ukweli, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama habari hizo zimehakikiwa mtandaoni.

ii) Wakati vyombo vya habari vya kawaida vinapotumia habari za mtandaoni, utambuzi kamili wa mwandishi wake ni lazima uonyeshwe katika habari inayotumika.

iii) Vinapotumia habari zote za mtandaoni, vyombo vya habari ni lazima viwataje kikamilifu walioandika habari hizo za mtandaoni.

iv) Habari zote za mtandaoni zinapotumiwa na vyombo vya habari vya kawaida ni lazima zizingatie sheria za tasnia ya habari na kanuni zinazoongoza chombo cha habari.

v) Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri itabidi wawajibikie kwa matokeo yoyote yale yatakayotokana na vyombo vyao kutumia habari hizo za mtandaoni.

Kanuni za Maadili kwa Afisa Uhusiano/Afisa Mawasiliano

2.0 Afisa Uhusiano/Afisa Mawasiliano

Katika shirika au taasisi, afisa uhusiano au afisa mawasiliano ni mkuu na kiungo cha mawasiliano, uhusiano na masuala mengine kati ya umma na shirika au taasisi husika. Wanawajibika kwa mawasiliano kwa kiwango kikubwa cha hadhira au watu tofauti, wote wa ndani na nje, vikiwemo vyombo vya habari, wafanyakazi na kwa utaratibu ili kutimiza kikamilifu majukumu yao kitaaluma na kimaadili, maafisa uhusiano na mawasiliano itabidi wazingatie: yafuatayo:

2.1 Uaminifu/Ukweli

Zingatia kwa kiwango cha juu usahihi na ukweli katika kuendeleza maslahi ya shirika au tassisi unayohudumia na katika kukuza mawasiliano kati yake na umma.

2.2 Haki

i) Toa huduma za haki kwa wateja, waajiri, washindani, wenzi, wachuuzi na wafanyabiashara ndogondogo kwa jumla hasa wa mitaani, vyombo vya habari na umma kwa jumla.

ii) Heshimu mawazo yote na kuunga mkono haki ya uhuru wa watu kujieleza.

2.3 Utetezi/Ukuzaji

Wakati wa kuendesha shughuli, kama ilivyo mawakili kwa makampuni yao, maafisa uhusiano watatoa maudhui ya viwango vya maadili ya taaluma ya tasnia ya habari nchini Tanzania.

2.4 Utiifu/Uaminifu

Wakati maafisa uhusiano na mawasiliano wanatakiwa

wawe waaminifu kwa makampuni yao, vile vile wana wajibu wa kutoa kwa wateja wao maudhui sawia yanayostahili.

2.5 Maelewano

Wana wajibu wa kutoa uelewano wa wote, staha na kukuza uhusiano kati ya taasisi na hadhira/umma.

2.6 Tunu za Taifa

Katika utekelezaji wa kazi zao wana wajibu pia wa kukuza na kulinda tunu za taifa ambazo ni amani, uhuru, umoja na usalama.

2.7 Uwajibikaji na wajibu

i) Maafisa uhusiano na mawasiliano watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kipaumbele chao badala ya shughuli zao, maslahi na uhuru binafsi.

ii) Watahesabu habari kama bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa. Vivyo hivyo watawajibika siyo tu kwa wale wanaothibiti au kumiliki vyombo vyao vya habari bali pia kwa umma na sehemu kubwa ikiwa maslahi ya jamii.

iii) Watawajibika na matokeo yatokanayo na vitendo vya taaluma yao au vitendo vilivyofanywa au kuchukuliwa kwa moyo, na kufanya maamuzi kwa weledi. Chini ya mazingira hayo watatekeleza wajibu wao kulingana na ufahamu wa maadili.

2.8 Maudhui ya habari za mtandaoni

i) Kwa maudhui ya habari zinazowekwa kwenye mtandao, maafisa uhusiano na mawasiliano wanapotumia habari hizo itabidi wawe makini na kujiridhisha pasipo mashaka maudhui yake ili kuhakiki ukweli, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama habari hizo zimehakikiwa na

mtandao.

ii) Wakati maafisa uhusiano na mawasiliano wanapotumia maudhui ya habari za mtandaoni, utambuzi kamili wa mwandishi wake ni lazima uonyeshwe katika habari inayotumika.

iii) Zinapotumika habari zote za mtandaoni, lazima wataje lazima viwataje kikamilifu walioandika habari hizo za mtandaoni.

iv) Habari zote za mtandaoni zinapotumiwa na maafisa uhusiano na mawasiliano ni lazima zizingatie sheria za tasnia ya habari.

v) Maafisa uhusiano na mawasiliano itabidi wawajibikie kwa matokeo yoyote yale yatakayotokana na kutumia habari za mtandaoni.

Kanuni za Maadili kwa Mawakala wa Matangazo wa Vyombo vya Habari

3.0 Mawakala wa matangazo wa vyombo vya habari

Mawakala wa matangazo wa vyombo vya habari ni makampuni, mashirika au watu binafsi wanaojitolea kutayarisha, kupanga na kushughulikia matangazo na njia nyingine zozote za kukuza wateja wao. Ili kutekeleza kazi zao kitaaluma na kwa maadili wanapaswa wazingatie na kudumisha yafuatayo:

3.1 Ukweli

i) Kusema kweli kwa jumla kuhusu bidhaa na huduma zinazotangazwa ili kuepuka kupotosha na kudanganya umma.

ii) Hakikisha bidhaa inayotangazwa inakidhi ubora unaotolewa na vyombo vinavyosimamia viwango vya ubora wa bidhaa.

iii) Epuka kukuza na kutangaza bidhaa ambazo kisheria zimepigwa marufuku na kuzuiliwa.

3.2 Lugha

i) Tumia lugha, alama na maumbo ambayo ni rahisi kueleweka na kutafsiriwa ipasavyo.

ii) Tumia maneno ambayo hayachochei na kusababisha watu kutoelewana na hivyo kuleta migogoro na migongano miongoni mwao au kusababisha madhara kwa jamii. Tumia lugha fasaha inayoleta amani na maelewano.

3.3 Uthibitisho

Uwe tayari kutoa ushahidi wa kuthibitisha madai

yoyote wakati mamlaka za usimamizi zinapotaka ufanye hivyo.

3.4 Vionjo na Heshima

Epuka maneno, taarifa na alama zenye kuleta uvunjifu wa amani na chuki kwa kundi lolote katika jamii.

3.5 Madai

Epuka madai yanayoweza kuwa ya kichochezi, upotoshaji na uongo.

3.6 Tunu za taifa

Epuka matangazo yanayotishia tunu za taifa za uhuru, amani, umoja na usalama wa taifa. Vivyo hivyo kuza matangazo ambayo yanatambua na kulinda haki na sifa za watu wengine.

3.7 Kashfa

Usitangaze tangazo au kukuza matangazo yenye kashfa na uzushi wa kuharibu majina ya watu.

3.8 Ubaguzi

Usitoe tangazo au kukuza matangazo yanayobagua kijinsia, ukabila, rangi, na wenye ulemavu wa aina yoyote ile.

3.9 Watoto

Usiwatumie watoto katika matangazo yanayohusu watu wakubwa. Pia epuka matangazo ya bidhaa zinazoleta madhara kwa watoto.

Maudhui

i) Usionyeshe vurugu au ukatili na uchokozi katika matangazo yanayolenga watoto.

ii) Usitangaze matangazo yanayoleta kero au yenye kauli mbiu za kutisha, picha au sauti za kuvuruga watoto.

iii) Usitangaze au kushawishi katika jamii tabia mbaya kwa watoto.

iv) Usishawishi watoto kuwaomba wazazi wanunue bidhaa zinazotangazwa na kuonyesha watoto wasio nazo kwa njia moja au nyingine wataonekana katika jamii kuwa ni fukara au watu wa chini.

Usalama

i) Usitangaze tangazo la kusema au kwa alama na michoro kuonyesha watoto wakishiriki katika vitendo visivyo salama au katika hali isiyo salama au tangazo linalowashawishi watoto kuingia katika maeneo mageni ya hatari isipokuwa tu kama ni ya usalama kwao.

ii) Usitangaze bidhaa zinazotumika katika hali isiyokuwa ya uslama, au bidhaa ambazo hazitakuwa salama zikitumiwa na watoto bila ya usimamizi, isipokuwa tu kama zimetangazwa mahsusi kwa ajili maalum ya usalama.

iii) Usionyeshe silaha bandia zinazioweza kutatanishwa na silaha halisi. Tunza vipindi vya matangazo kwa miezi ipatayo mitatu kwa ajili ya uhakiki iwapo kutakuwa na malalamiko kutoka kwa wasikilizaji au watazamaji.

3.10 Vileo, Tumbaku, Usalama Barabarani na Mazingira

Zingatia kanuni za miiko ndani za chombo husika cha utangazaji, ili kabla ya kukubali kupokea au kurusha matangazo ya bidhaa ihakikishwe bidhaa hizo hazina wasi wasi wa hatari ya madhara ya afya, usalama na mazingira.

3.11 Uwasilishi

Katika kutangaza baadhi ya bidhaa, eleza wazi kama

ukusanyaji wake au vitu vya ziada, (kama betri au manukato) vinahitajika kabla ya bidhaa za aina hiyo hazijatumika au ili kufanya bidhaa hizo zitoe matokeo yaliyokusudiwa na tangazo.

3.12 Mashindano

Eleza wazi kanuni za shindano linalotangazwa. Thamani yake na fursa za kushinda zisitiwe chumvi.

3.12 Matangazo ya Utata na Kisiasa

Uwe makini na matangazo yenye masuala ya utata kama propaganda za kisiasa na masuala yanayohusiana na imani ili kuhakikisha tangazo kama hilo haliingilii haki za watu wengine.

Matangazo kutoka kwa wadhamini au yaliyolipiwa yatofautishwe na habari.

3.13 Udhamini

i) Kubali udhamini tu kutoka mashirika yanayokubalika kisheria na kijamii. Tangazo lolote kutoka kwa mdhamini litofautishwe na habari.

ii) Epuka matangazo yanayohatarisha afya na ustawi wa jamii.

iii) Epuka tangazo linaloweka rehani na kuteka taaluma au kuathiri ubora na uadilifu hasa wa chombo husika cha habari.

3.14 Kanuni za Maadili

Tangazo lisipingane na miiko ya maadili yanayozingatiwa na wanataaluma wa habari.

3.15 Tangazo la Ushuhuda

Tangazo la ushuhuda halitakuwa na nguvu kwa mashuhuda wenye uwezo wa kuelezea hali halisi au maoni ya ukweli au uzoefu katika tangazo husika.

3.16 Uwajibikaji na wajibu

i) Watatambua wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kipaumbele chao badala ya shughuli zao, maslahi na uhuru binafsi.

ii) Watahesabu habari kama bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa. Vivyo hivyo watawajibika siyo tu kwa wale wanaodhibiti au kumiliki vyombo vyao vya habari bali pia kwa umma na sehemu kubwa ikiwa maslahi ya jamii.

iii) Watawajibika kwa matokeo yatokanayo na vitendo vya taaluma yao au vitendo vilivyofanywa au kuchukuliwa kwa moyo, hiari na maamuzi yake kuchukuliwa kwa weledi. Chini ya mazingira hayo watatekeleza wajibu wao kulingana na ufahamu wa maadili.

3.17 Maudhui ya habari za mtandaoni

i) Kwa maudhui ya habari zinazowekwa kwenye mtandao, watangazaji wa matangazo wanapotumia habari hizo itabidi wawe makini ili kuhakiki ukweli, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama habari hizo zimehakikiwa na mtandao.

ii) Wakati watangazaji wa matangazo wanapotumia maudhui ya habari za mtandaoni, utambuzi kamili wa mwandishi wake ni lazima uonyeshwe katika tangazo linalotumika.

iii) Watawajibika kwa matokeo yoyote yale yatakayotokana na kutumia habari za mtandaoni.

Kanuni za Maadili kwa Watangazaji

4.0 Watangazaji

Mtangazaji ni mtu, kampuni au shirika, mtandao au kituo kinachorusha matangazo ya vipindi vya redio au runinga. Utangazaji una aina mbalimbali ya wafanyakazi wakiwemo wasomaji, waandishi wa habari wa runinga na radio, wapiga picha, waandishi wa muongozo(waongozaji), wahifadhi sauti, wasimamizi wa vipindi, wahariri na wanamawasiliano wanaofanya kazi na vyombo vya habari vya redio na runinga. Katika kufanya kazi zao ipasavyo kitaaluma na kimaadili, watangazaji ni lazima waongozwe na miiko ambayo ni kanuni za kimaandili na taaluma. Hapa kuna baadhi ya kanuni muhimu ambazo zinapaswa kuzingatiwa na mtangazaji na mwandishi wa habari mtangazaji. Wanataaluma watangazaji ni lazima waongozwe na kanuni za maadili na taaluma. Hapa ni baadhi ya kanuni muhimu ambazo mtangazaji na mwandishi hana budi kuzingatia:

4.1 Kanuni za Maadili

4.1.1 Tafuta ukweli na utangaze

i) Atasoma kwa uwazi, mahususi na ukweli matukio kama ilivyoelezwa na vyanzo vyote kuhusiana na kiini cha tukio husika.

ii) Hatatoa taarifa za uongo na zilizotengenezwa zinazokusudia kudanganya hadhira, kupotosha ukweli au zenye nia mbaya.

4.1.2 Uwajibikaji na Wajibu

i) Watangazaji watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kipaumbele chao badala ya mambo

binafsi ya shughuli zao, maslahi na uhuru.

ii) Wataichukulia habari kama bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa. Vivyo hivyo watajibika siyo tu kwa wale wanaodhibiti au kumiliki vyombo vyao bali pia kwa umma na sehemu kubwa ikiwa maslahi ya jamii.

iii) Watawajibika kutokana na matokeo yatokanayo na vitendo vya taaluma yao au vitendo vilivyofanywa au kuchukuliwa kwa moyo, na maamuzi yake kuchukuliwa kwa weledi. Chini ya mazingira hayo watatekeleza wajibu wao kulingana na ufahamu wa maadili yao.

4.1.3 Kuzuia madhara

i) Watangazaji wataheshimu vyanzo vyao, wasikilizaji, wafanyakazi wenzao, na umma kwa jumla katika jamii kama binadamu wanaohitaji kuheshimiwa.

ii) Wataonyesha huruma kwa wale ambao huenda wameathirika na uandikaji wa habari zao. watakuwa makini zaidi wakati wanashughulikia watoto na vyanzo visivyo na ujuzi au watu wengine.

4.1.4 Kufanyakazi kwa kujitegemea

Watawasilisha taarifa ya habari waliyoipata kwa misingi ya ukweli bila hofu ya kuadhibiwa na bila kushawishiwa na watu binafsi, makundi yenye maslahi au watu wengine wa ndani na nje.

4.2 Viini vya tunu

4.2.1 Ukweli/usahihi

i) Watawasilisha tu taarifa ya habari yenye

ukweli na uhakika ambayo imehakikiwa pasipo mashaka kuhusu uhalali na usahihi wake.

ii) Wataarifu ukweli upasao wa muktadha kwa kutoa siyo tu ukweli kuhusu suala husika bali pia na mazingira ya muktadha wa suala hilo.

4.2.2 Uadilifu/mizania/haki

i) Watawasilisha kwa uwazi masuala bila kuwa upande wowote wa wahusika.

ii) Watazipa haki pande zote katika suala husika fursa sawa ya kutoa mambo yao katika habari hiyo. Tafuta na uweke kauli binafsi za waathirika.

iii) Wataupa kila upande (unaodai na kutuhumiwa) muda sawa wa kutoa maelezo yao.

4.2.3 Ukweli/uadilifu

i) Watangazaji watafanya kazi yao kwa mujibu wa kanuni za taaluma ya uandishi wa habari na kwa mujibu wa viwango vya haki na makosa.

ii) Wataacha kushiriki kwenye shughuli ambazo ziko kinyume na maadili na kanuni za taaluma zinazowafunga

4.3 Vionjo na Heshima

Vionjo ni suala linalotofautiana sehemu moja hadi nyingine katika jamii kutegemeana na mahali walipo watangazaji husika na hivyo kuwa vigumu kwao kuweka viwango vya vionjo vinavyokubalika na hadhira yote. Heshima inahusu kuheshimu mila na misingi ya imani za jadi za watu. Suala la vionjo na heshima pia linapokelewa kitofauti kutegemea na

taswira ya mtu. Kwa hiyo, kwa watangazaji ili kudumisha vizuri vionjo na heshima ni lazima wazingatie yafuatayo:

i) Kutambua na kuzingatia kanuni, sheria na viwango vya heshima vinavyokubalika na mamlaka za usimamizi wa eneo ambalo watangazaji wanafanya kazi.

ii) Kufikiria muktadha ambao lugha na tabia hutokea(ukiwemo ucheshi, tashtiti na mambo mengine ya kuvutia), na wakati wa kurusha matangazo na hadhira (wasikilizaji na watazamaji) ya kipindi husika.

iii) Kuwatendea haki kwa heshima watu na vyanzo vyao. Watakuwa makini zaidi wakati wakishughukia watoto.Watajitahidi kadri iwezekanavyo na kwa tahadhari wakati wakiwa nao kwa mahojiano na kuweka vifaa vya utangazaji kwa namna isiyoweza kuwa pingamizi au kizuizi kwa watoto.

iv) Kila mara toa onyo kwa tahadhari kama kipindi kina vitu ambavyo huenda vikaogofya baadhi ya watu.

4.4 Maelezo Hatari au Tabia Mbaya

i) Wasirushe kwa undani zaidi picha au habari kuhusu njia za kujiua au kujinyonga, kutengeneza vilipuzi, au matumizi ya dawa za kulevya, vitendo ambavyo huenda vikaelekeza au kushawishi baadhi ya watu kuvifanya.

ii) Waepuke kutangaza kipindi chochote cha kuigiza ambacho habari au matukio yake kwa sauti au picha yanapotosha au kutisha wasikilizaji au watazamaji.

iii) Wasionyeshe kipindi chenye mchakato wenye halisia ya mazingaombwe ya kumpumbaza mtu

au mchakato unaolenga kushawishi hali ya kupumbaza mtu afanye kitu asichokijua na hivyo kupotosha au kuleta hofu kwa hadhira..

4.5 Unyeti wa Jinsia

i) Watangazaji waepuke matumizi ya maneno na maelezo ya mawazo mgando ambayo yataonyesha kuwa jinsia moja ni dhaifu kuliko nyingine kwani maneno hayo yakitumika mara kwa mara yatajenga dhana miongoni mwa watu kwamba kuna jinsia moja dhaifu katika jamii.

ii) Watoe taarifa kama tu ina uhusiano wa suala lolote kuhusu ukabila, rangi ya mtu, dini, mapenzi ya jinsia na hadhi ya ndoa, athari za kimwili au akili au aina yoyote ya ulemavu.

4.6 Uhalifu na Vurugu

Kisitangazwe kipindi kinachoelekea kukuza raia kutotii amri au sheria bila shuruti, kushawishi uhalifu au kukuza aina nyingine za maovu ya utu.

4.7 Machafuko na huzuni

i) Watangazaji wasihalalishe machafuko yanayoonyeshwa kutokana na uzito wake kwa picha au sauti kama muhimu kwa muktadha wa kipindi.

ii) Wasirushe mambo ya ukatili na unyasasaji wa kijinsia katika namna inayolenga kusisimua hadhira. Maelezo wazi zaidi na mtazamo wa muda mrefu kwenye ukatili wa kimwili ni lazima viepukwe.

iii) Waangalie katika kuamua kama waingize maelezo zaidi ya alama zinazohusu uzito wa ukatili kwa jumla na msaada unaohitajika kuelewesha watu kuhusu suala hilo.

iv) Wafikirie kwa maknini urushaji wa picha zinazohuzunisha zikiwemo za:

a) Mateso au kutendewa vibaya kwa watu na wanyama

b) Picha za watu waliokufa na miili kukatwa katwa vipande

c) Picha za watu walioko katika uchungu mkubwa au wanakaribia kufa.

d) Ukatili au kutendewa vibaya watoto.

4.7 Onyo na Kuvuruga au Uvunjivu wa Maudhui

Watangaze maonyo kabla ya kuanza kipindi chochote chenye lugha au picha za kuleta hofu au za kusababisha kuvuruga watazamaji au wasikilizaji wa kawaida.

4.8 Kashfa

i) Hawatatangaza kitu wala kukikuza kitu kilicho na maudhui ya kashfa na hivyo kuwa pia adha na kero kwa watazamaji na wasikilizaji.

ii) Hawatasema moja kwa moja maneno kuhusu mtu au kitu kwa nia ya kushusha hadhi ya mtu. Wala kugeuza maneno kwa njia ambayo watazamaji na wasikilizaji kutokana na maelezo ya habari hiyo watahisi ni fulani.

4.9 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Utendaji wa Wahariri

i. Vitendo vya Upotoshaji

Zisifanyike mbinu za udanganyifu katika kuanda kipindi iwe kwa vitendo au kiufundi kwa kutumia vitu ambavyo kihalisia hata kwenye maktaba ya filamu au mikanda hivyo havipo.

ii. Mahojiano/Simu/Majadiliano

a) Mahojiano lazima yasifanyiwe majaribio kwanza na maswali maalum yasipelekwe kwa

mhojiwa. Inaruhusiwa kujadiliana mapema na mhojiwa kuhusu masuala ya mahojiano.

b) Watangazaji wapange, waendeshe na kuhariri kwa haki na ukweli mahojiano, uchambuzi, mikutano na majadiliano kwa ajili redio na runinga.

c) Wasipotoshe au kuwasilisha isivyo halali maoni ya washiriki au kutoa taswira potofu ya mazungumzo.

d) Wasiwasilishe mambo yaliyokuwa yamerekodiwa na kuonyesha kama mahojiano, uchambuzi, mikutano na majadiliano mubashara.

e) Watoe tahadhari mapema kwa wapiga simu kuhusu kurekodi simu zao zinazoingia ili kuepuka matumizi ya lugha mbaya, kashfa, ubaguzi na dharau kwa jinsia na makundi mengine.

f) Kwa kawaida tangu mwanzo watangazaji wanapaswa wajitambulishe kwa wanaowahoji kwa simu, au wakubaliane kama wanataka mazungumzo ya simu yanarekodiwa ili yatangazwe.

iii. Vibonzo

a) Usiweke kwenye kipindi vibonzo vyenye machafuko ya kupindukia au utesaji kuonyesha hulka za binadamu

b) Usionyeshe vibonzo vinavyoshambulia watu kwa misingi ya rangi, imani za dini na mapenzi kinyume na maumbile

iv) Haki katika Ushindani

Katika vipindi na promosheni zinazotoa zawadi au tuzo hakikisha hakuna hila ya ushirikiano kati ya watangazaji na washindani ili kutenda haki kwa

pande zote na kuepuka upendeleo kwa upande mmoja.

4 .10 Matangazo ya Kutangazwa:

i) Wakati wa kutangaza matangazo, fanya hivyo kwa mujibu wa kanuni za kitaaluma za mwandishi wa habari pamoja na kwa mujibu wa sheria na kanuni za Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania TCRA zinazotawala vyombo vya habari.

ii) Epuka kushiriki katika shughuli zozote ambazo ni haramu na kinyume cha imani za kitaaluma.

iii) Weka ukomo wa matangazo ya kila siku kwa wastani wa asilimia 30 ya muda wote wa kwenda hewani.

iv) Udanganyifu

a) Usipotoshe hadhira au watu kwa utata au athari kutokana na sauti au picha.

b) Linganisha kwa haki bidhaa zinazotangazwa kwa misingi ya ukweli unaoweza kuzithibitishia.

c) Kwa njia yoyote ile usitumie tangazo ambalo litadhalilisha au kushusha hadhi ya washindani au bidhaa.

d) Ushahidi wa kweli utolewe na kuungwa mkono kwa kuelezea uzoefu wa mtu binafsi anayetoa ushahidi au kuunga mkono kitu hicho. Mtoto aistumike katika mambo hayo.

v) Dhamana

a) Kuwa makini na matangazo yenye dhamana kuhakikisha huduma inayoahidiwa inapatikana kama inavyoonyeshwa kwenye matangazo yake.

b) Usieleze bidhaa au huduma kuwa za 'bure' isipokuwa tu kama bidhaa au huduma hizo zinatolewa bila gharama au gharama ya ziada

mbali na gharama za posta au usafirishaji.

vi) Mtangazo yenye Utata na Siasa

a) Eleza kwa uwazi utambulisho wa mteja ambaye tangazo lake linashughulikia jambo lenye utata wa maslahi ya umma, siasa au kampeni halisi au dira.

b) Kwa njia yoyote ile vyombo vya habari visitoe kamisheni, punguzo au vishawishi vingine kwa watu binafsi au makundi yanayojihusisha na tabia mbaya inayoharibu maadili na taaluma.

vii) Watoto

Usitangaze matangazo ya watu wazima wanaotumia watoto. Pia watoto wasiwekwe rehani kwa matangazo yanayowadhuru.

Maudhui

a) Usitangaze tangazo lenye maudhui yanayoonyesha vurugu na uchokozi unaowalenga watoto.

b) Usitangaze matangazo yenye kauli mbinu zinazoleta kero au kuogofya, picha au sauti zinazovuruga na kuwaogofya watoto.

c) Usitangaze au kushawishi tabia mbaya ya jamii inayofanywa na watoto.

d) Usishawiji watoto kuomba wazazi wao kununua bidhaa zinazotangazwa, wala mtangazaji mwenyewe usionyeshe kwamba watoto ambao hawamiliki au hawana bidhaa kama hizo ni dhalili, fukara na wa hali ya chini katika jamii.

Usalama

a) Usitangaze tangazo lolote lile liwe kwa

mdomo au alama kuonyesha watoto wakishiriki katika vitendo visivyo salama au wako katika hali isiyo salama, au maudhui yanayowashawishi waingie maeneo mageni hatari isipokuwa tu kama ni tangazo maalum la usalama kwa watoto.

b) Usitangaze bidhaa zinazotumika kwa namna isiyo salama au hatari, au bidhaa ambazo hazitakuwa salama iwapo zitatumika na watoto bila usimamizi, isipokuwa tu ziwe mahsusi kwa usalama wa watoto.

c) Usionyeshe silaha bandia ambazo zinaweza kutatanishwa na silaha halisi za kawaida.

d) Kwa tahadhari weka kwa miezi mitatu vipindi vyenye matangazo kwa minajili ya kufanya uhakiki iwapo baadaye kutakuwa na malalamiko kutoka kwa wasikilizaji/ watazamaji.

viii) Vileo, Tumbako, Usalama na Mazingira

Kabla ya kukubali au kurusha matangazo ya bidhaa zinazogusa mambo ya afya, usalama, mazingira au wasiwasi mwingine, zingatia kanuni za ndani za chombo husika cha habari

ix) Uwasilishi

Katika utangazaji wa baadhi ya bidhaa ielezwe wazi kama mkusanyiko au ziada ya vitu, (kwa mfano betri au manukato), vinahitajika kabla ya bidhaa hizo kutumika au ili kutoa athari iliyotangazwa ya bidhaa hizo. Usidharau kiwango cha uwezo wa watoto kutumia bidhaa hizo. Kinachotakiwa ni kuwajengea uwezo kulingana na umri wao ili kufikia malengo yaliyosukudiwa ya bidhaa husika inayotangazwa.

x) Mashindano

Katika maudhui ya utangazaji yanayohusiana na

mashindano, eleza wazi kanuni za shindano husika. Thamani yake na nafasi za kushinda shindano zisitiwe chumvi.

xi) Matangazo ya Utata na Kisiasa

Unapotangaza masuala ya utata kama propaganda za kisiasa na masuala yanayohusiana na dini, epuka maudhui ya yasiingilie haki za watu wengine.

xii) Udhamini

i) Ukubaliwe tu udhamini kutoka taasisi zinazokubalika kisheria na kijamii.

ii) Epuka kutangaza matangazo yanayohatarisha afya na ustawi wa jamii

iii) Epuka kutangaza mtangazo yanayoweka rehani taaluma au kuathiri ubora na uadilifu hasa wa chombo husika cha habari.

iv) Katika utangazaji wa matangazo kutoka kwa wadhamini au yaliyolipiwa, watangazaji watofautishe maudhui ya matangazo na ya habari.

4.11 Uchambuzi, Maoni na Tahariri

Matangazo yote lazima yawe na msingi wa kutosha wa habari na maelezo ya kuwezesha hadhira/watu ambao ni watazamaji na wasikilizaji kuelewa umuhimu na matokeo ya habari iliyotangazwa. Wakati wowote waandishi wa habari wasiweke maoni au maamuzi binafsi katika habari.

i) Vipindi vinavyohusu masuala nyeti ya umma, tunu za taifa, programu za masuala ya umma na maoni vitashughulikiwa tu na watu wenye maarifa sahihi kupitia mafunzo waliyopata na utendaji wao kutokana na maadili ya utangazaji. Kwa upande mwingine, wazungumzaji waalikwa katika vipindi lazima wawe watu wenye uwezo

na sifa katika suala linalohusika.

ii) Vipindi vya masuala ya umma vinavyotangazwa katika muda uliofikiwa kwa mkataba na pande nyingine majina ya wahusika wanaowajibika kwa utayarishaji wake kila wakati vinaporushwa hewani yatatajwa.

iii) Pande pinzani au zinazogongana katika masuala ya umma ni lazima zipewe haki sawa katika kutetea maoni yao.

iv) Upendeleo binafsi au maoni visiruhusiwe kuvuruga mambo ya ukweli.

4 .12 Habari zinazohusisha watoto

Wakati wote hadhi ya mtoto ni lazima iheshimiwe. Mtoto asidharauliwe au kudhalilishwa na kutokuwa kwake na hatia kuheshimiwe.

i) Mazingira binafsi ya mtoto ya kuleta kashfa lazima yaepukwe. Iwepo juhudi ya ufahamu kuepuka kashfa, mawazo mgando, hisia au kutumika kwa watoto wenye ulemavu, watoto walioko katika makundi ya watu wachache na ya wazawa.

ii) Haki ya faragha ya watoto kila mara ni lazima iheshimiwe. Kwa vile uenezi usiostahili au kashfa kunaweza kuwaletea madhara, watoto ambao ni waathirika wa udhalilishaji au mgongano wa sheria, ni lazima wasitambulishwe moja kwa moja au kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Taarifa yoyote ambayo huenda ikawasababishia kutambuliwa isitangazwe.

iii) Kuwa hatari kwa watoto kunahitaji ulinzi maalum kutoka kwa watangazaji, licha ya hadhi au vitendo vya wazazi wao. Ni lazima kusiwe na udhalilishaji wa watoto kutokana na ghiliba na imani yao. Wala wasiulizwe kuhusu mambo ya faragha ya kifamilia au mambo mengine yaliyo chini ya uelewa wao.

Kuhusu mambo muhimu ridhaa ya wazazi lazima ipatikane kabla ya kuhojiwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18.

iv) Mahali ambapo ridhaa haikupatikana au kwa ukweli imekataliwa; ni maslahi ya umma ndiyo yanaweza kuhalalisha uamuzi wa watoto wenye umri ya chini miaka 18 kuhojiwa bila ridhaa ya wazazi. Vivyo hivyo watoto wenye umri wa chini ya umri 18 wanaohusika katika uchunguzi wa polisi au mienendo ya mahakama kuhusiana na masuala ya kijinsia hawatajwa majina katika habari au vipindi vingine.

4.13 Haki ya kujibu

i) Watangazaji watatoa fursa ya haki ya kujibu kwa watu binafsi, makundi au taasisi wanapotakiwa kwa sababu zinazohitajika. Kupitia vyombo vyao vya habari, mara moja na kwa umuhimu wake, watangazaji watatangaza masahihisho ya makosa yaliyofanyika.

ii) Watatoa nafasi sawa zinazostahili kwa pande zote kutoa maoni yao wakati wa kushughulikia masuala ya utata yenye umuhimu wa umma, au ndani ya kipindi hicho hicho au vinavyolingana, iwapo suala husika lina umihimu wa kipekee katika jumuiya au jamii.

iii) Wala (watangazaji) hawataeleza kinyume maoni yaliyotakiwa katika kipindi wala mambo mengine kwa namna ya kupotosha kwa kutoa makosa au kusisitiza kitu isivyostahili au kuhariri muktadha wake.

4.14 Faragha

Watangazaji wasitumie vitu vinavyohusiana na masuala ya mtu binafsi au faragha, au yanayoingilia faragha ya mtu binafsi, isipokuwa tu kama kuna maslahi ya juu

ya umma katika kutangaza habari kama hiyo.

4.15 Vipindi vya moja kwa moja vya Simu

i) Vipindi vya moja kwa moja vya mahojiano ya simu ni njia maarufu sasa inayokubalika kutangaza maoni ya watu binafsi. Hata hivyo, tahadhari ni lazima ichukuliwe kudumisha kanuni za haki, uadilifu, lengo lake na kuwepo mizania kwa ajili ya kupanua wigo wa aina mbalimbali za maoni.

ii) Watangazaji wa vipindi wanatakiwa kusimamia majadiliano na siyo kuwa chombo tu cha kurushia hewani maoni binafsi ya watu kwa hiyo ni lazima kuwatendea haki wanaopiga simu. Zaidi ya hayo, vipindi ni lazima vilindwe ili visiingiliwe na makundi shinikizi yaliyojiandaa kufanya hivyo au watu binafsi wasiowajibika.

4.16 Hali ya Usimamizi na Heshima

i) Wakati wote katika matangazo ya Redio na Runinga, vikiwemo vipindi vya mazungumzo na midahalo, idumishe hali ya utulivu na taaluma na kuonyesha mfano wa ustaarabu, mhadhara unaoheshimika, pamoja na heshima kwa ajili ya haki za binadamu kwa watu wote.

ii) Matangazo yasiwe na vitu ambavyo vitachukuliwa kama ni uchochezi wa vurugu.

iii) Vipindi vya vurugu au hali nyingine tete lazima vidhibitiwe na mizania ya ukweli.

4.17 Masuala yanayohusiana na Imani

i) Watangazaji na wageni inawabidi wasifanye fedheha au aibu kwa masuala ya dini, ukabila, jamii na uchumi au utamaduni yanayomhusu mtu yoyote binafsi au makundi na kuzingatia mambo ya kimsingi ya maadili.

ii) Wachangiaji na wahubiri katika vipindi vya dini hawapaswi kukuza maoni yao kwa njia isiyotakiwa, wala wasishambulie madhehebu na imani nyingine.

4. 18 Kuepuka Uragbishi

Uhuru, demokrasia na haki za binadamu havina budi kulindwa. Hata hivyo, hiyo haina maana ya kupigia chapuo upitishaji wa sera mahsusi au sheria, au kuridhia au kupinga wagombea wa kuchaguliwa au kuteuliwa.

4.19 Viwango vya Kuhariri na Kutayarisha vipindi

Watu wote wanaohariri habari, mahojiano na mambo mengine ya kwenda hewani watahakikisha uhariri wao unaonyesha haki, ukweli na bila kuchanganya kilichosikilizwa na kusikika.

i) Mahojiano yahaririwe kwa namna ya kudumisha hata makali na machungu yaliyomo katika mahojiano.

ii) Majibu yasiondolewe katika muktadha au kuhaririwa kwa namna ya kubadili maana yake.Usimulizi wa makali yanayouma lazima uonyeshe swali lililosababisha majibu hayo.

4.20 Haki za kunakili

Watangazaji inawabidi waheshimu haki ya kunakili na uwajibikaji wa haki za jirani kwa suala zima la kuheshimu kitu chochote cha nje katika utangazaji.

4.21 Wizi wa Maandishi na Mawazo

Usitumie maandishi au mawazo ya mtu mwingine bila idhini yake na kueleza bayana chanzo halisi unapotumia maandishi au mawazo hayo.

4.22 Maudhui ya Mtandaoni

a) Watangazaji wanapotumia maudhui au mambo ya mtandaoni wahakiki maudhui yake pasipo mashaka ukweli wake, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama mambo hayo yalihakikiwa na mtandao husika.

b) Wakati watangazaji wanapotumia maudhui ya mtandaoni ni lazima wazingatie sheria na kanuni za tasnia ya habari.

c) Wakati watangazaji wanapotumia maoni ya maudhui ya mtandaoni ni lazima wawajibike kikamilifu kwa matokeo yatakayotokana na mambo yaliyotumiwa.

Kanuni za Maadili kwa Wapiga picha wa magazeti na Wasimamizi wa Video

Mpiga picha wa gazeti ni mwandishi wa habari aliyefundishwa kupiga picha za matukio na kutumia picha zake kwa mawasiliano.

Msimamizi wa Video:

Ni mtu anayesimamia mchakato wa kutengeneza video wakati mtayarishaji wake ni mbunifu wa mradi wa utengenezaji wa video hiyo. Anasimamia tangu kubuniwa kwake hadi ukamilishaji wa mradi huo. Ili kutekeleza majukumu yao kitaaluma na kwa maadili, wapiga picha za magazeti na wasimamizi wa video hawana budi kuzingatia yafuatayo:

5.1 Kanuni za Maadili

i. Tafuta na uwasilishe ukweli

a) Wapiga picha za magazeti na wasimamizi wa video watachapisha au kutoa picha zinazoonyesha usahihi wa hali ya tukio

b) Wasitoe ukweli bandia kwa kutumia vifaa vyovyote vile kama jicho la kamera, vichuja mwanga, eneo la kukaa ili kupata picha nzuri, kupiga picha katika hali unayoitaka, kutumia kompyuta na mbinu nyingine za kiufundi za kubadili hali halisi ya ukweli wa picha.

c) Wahamishe picha zilizopigwa kwa namna inavyolingana na muktadha wake kwa kutoa siyo tu picha yenyewe bali pia muktadha wa mazingira yake.

ii) Uwajibikaji na wajibu

Uwajibikaji na Wajibu

a) Wapiga picha za magazeti na wasimamizi wa video watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kuwa kipaumbele chao badala ya shughuli zao za kawaida, maslahi na uhuru binafsi.

b) Watahesabu habari kama bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa. Vivyo hivyo watawajibika siyo kwa wale wanaodhibiti au kumiliki vyombo vyao vya habari bali pia kwa umma na sehemu kubwa ikiwa maslahi ya jamii.

c) Watawajibika kwa matokeo yatokanayo na vitendo vya taaluma yao au vitendo vilivyofanywa au kuchukuliwa kwa dhamira, na kuchukua maamuzi kwa weledi. Chini ya mazingira hayo watatekeleza wajibu wao kulingana na ufahamu wa maadili yao.

iii) Kuzuia madhara

c) Wawe makini wakati wanapochukua na kutumia picha za walioathirika na majanga au watu wenye huzuni. Picha za aina hiyo zitatumika inapokuwa lazima kuelezea habari iwapo njia nyingine zote zikiwa zimeshindikana.

iv) Kuwa huru

Wataripoti taarifa walizopokea kwa misingi ya ukweli na bila hofu ya kuadhibiwa na bila kushawishiwa na watu binafsi, makundi yenye maslahi au watu wengine wa ndani na nje.

5.2 Tunu muhimu

i) Uhalisia wa kweli/usahihi

a) Hali inayoonyeshwa katika picha iwe ya haki na ukweli kutokana na uwekaji sahihi wa matukio, maudhui na sauti.

b) Watoe tu picha za uhalisia na video ambazo zimehakikiwa pasipo mashaka kuhusu uhalali na usahihi wake.

5.3 Uadilifu wa taaluma

i) Watafanya shughuli zao kwa mujibu wa kanuni za taaluma na kwa mujibu wa viwango vya haki na makosa.

ii) Wataepuka kushiriki katika shughuli ambazo ziko kinyume na imani za taaluma yao.

iii) Kudumisha, kutekeleza na kuzingatia viwango vya juu vya tabia na kanuni za mwenendo ili kudumisha na kulinda uadilifu na uhuru wa taaluma. Watajitambulisha wenyewe na vyombo vyao vya kazi. Kamwe hawatatumia njia za vificho au ghiliba ili waingie sehemu zilizokatazwa.

iv) Hawatapiga picha bila kibali au kutumia vitambulisho vya waandishi wa habari ili kupata fursa ya kuingia sehemu zilizozuiliwa kama sehemu za sherehe, dansi, mikutano na shughuli nyingine za binafsi. Vivyo hivyo hawatatumia vitu hivyo kupata upendeleo wa aina yoyote ile.

v) Hawatahujumu kwa makusudi juhudi za waandishi wa habari wengine.

5.4 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Uhariri

i.) Uchezeaji wa picha

a) Usifanyike uchezeaji au ubadilishaji wa picha ya gazeti au video isipokuwa katika matukio ambayo kisheria, kimaadili na kwa hali halisi yanaruhusiwa.

b) Iwapo kwa sababu maalum picha inabadilishwa au zinakuwepo nyongeza, mabadiliko hayo itabidi yaelezwe kwa watazamaji na sababu hizo za kufanywa

mabadiliko hayo zitajwe kama sehemu ya habari.

c) Picha mpya zisibadilishwe kwa njia ambayo itavuruga ukweli, kupotosha watazamaji au kuwasilisha vibaya wahusika wa picha hizo.

d) Uimarishaji wa picha kwa uwazi wa kiufundi kama uhariri, kupunguza picha na mambo mengine ya kiufundi kila mara ni vitu vinavyoruhusiwa lakini udumishwe uadilifu, maudhui ya picha na muktadha.

ii) Ubaguzi

a. Epuka kuchukua na kutoa picha za magazeti na video ambazo zinabagua watu binafsi na makundi.

b. Tambua na kufanya kazi ili kuepuka upendeleo wa mtu mmoja katika kazi.

c. Watendee watu wote kwa heshima na hadhi. Toa upendeleo maalum kwa watu walio katika hatari na huruma kwa waathirika wa uhalifu au majanga.

iii) Haki ya Faragha

Heshimu haki za raia kwa jumla kuhusu faragha, nafasi na habari za binafsi. Hata hivyo, haki ya faragha haitaingilia uchukuaji picha za magazeti na video kwa ajili ya kumbukumbu za umma, au mambo mazuri kwa jumla kwa jamii.

iv) Masahihisho

Kiri makosa kwa maelezo ya undani zaidi na kuhakikisha picha zenye makosa zilizochapishwa au kutangazwa zinasahihishwa mara moja, na kutoa masahihisho kwa nafasi kama ile ya makosa yanayosahihishwa.

v) Huzuni

a) Heshimu huzuni binafsi kwa kutolazimisha

mahojiano na watu walio katika huzuni ya msiba ama janga. Waandishi wa habari wachukue tahadhari ya kuacha kuwaongezea maumivu na huzuni zaidi watu waliopoteza wapendwa wao kwa kushinikiza kufanya nao mahojiano. Waandishi wa habari pia waheshimu mtu aliyefariki. Uandishi wa habari za matukio ya misiba usizidishe maumivu kwa waliopoteza wapendwa wao.

b) Wanahabari wahughulikie kwa makini hali za huzuni kutokana na hali ngumu ya walioathirika wa janga na msiba. Wakati wakipiga picha, wasifanye kitu chochote kitakacho zidisha uchungu na huzuni kwa watu wasio na hatia, waliofiwa na wengine walio katika huzuni. Vivyo hivyo waandishi wasiingilie nyakati za faragha za huzuni isipokuwa pale maslahi ya umma yanapohalalisha kuonekana kwa tukio hilo la huzuni.

c) Chukua tahadhari maalum wakati unachukua na kutoa picha za marehemu. Usichukue wala kuchapisha picha za aina hiyo bila kibali cha ndugu. Wakati unashughulikia picha za hali ya aina hiyo, kila mara fikiria utamaduni, visasili, imani na mila za watu wanaohusika na msiba huo.

vi) Picha chafu

Usichukue picha za utupu, na inapotokea picha za aina hiyo haziwezi kuepukwa, basi usiangazie viungo vya siri, au hali zinazodhalilisha na kushusha hadhi ya watu.

Marekebisho zaidi ya picha yanakubalika ikiwemo kuzipunguza na kubadilisha rangi.

vii) Picha za maumivu ya kibinadamu/waathirika wa

machafuko

Usiwe mpenda ukatili na utesaji kwa kubeza maumivu ya kibinadamu na kuchukua picha za matukio kama hayo bila kujisikia utu. Vivyo hivyo, kila iwezekanavyo usichukue picha, na kuacha waathirika kwenye mateso bila kutoa msaada ikiwemo kuwafariji kuwapoza machungu waliyonayo.

viii) Kupanga matukio

Wapiga picha na wasimamizi wa vipindi wasipange matukio. Wanapopiga picha za washiriki wa kipindi ndani ya studio, waepuke kuwapotosha watazamaji kuamini picha hizo zilichukuliwa wakati wa ukukusanyaji habari husika. Mabadiliko yoyote ya picha sharti yaonyeshwe ili isionekane kumekuwepo jaribio la kudanganya.

ix) Masuala ya Kijamii yenye Mshtuko na Hisia kali

Wapiga picha wawe waangalifu wakati wanaposhughulikia masuala ya jamii hasa yenye hali ya mshtuko au mhemuko wa hisia kali kama maafa, machafuko, matumizi ya dawa za kulevya, ukatili, kupenda ukatili na utesaji na picha chafu hasa za ngono. Tumia picha za hali hiyo tu iwapo imeshindikana kupata njia nyingine za kuelezea habari husika. Sababu za kutumia picha kama hizo lazima zielezwe.

x) Wizi wa maandishi na mawazo

a) Wapiga picha na wasimamizi wa vipindi vya video waepuke kujihusisha na wizi wa maandishi na mawazo. Wizi wa maandishi na mawazo unahusu kutumia vitu au mawazo ya mtu mwingine bila kibali chake na kumtaja mhusika na mawazo hayo.

b) Maelezo ya kumtaja mhusika pia yatolewe kwa picha zilizochapishwa au kutangazwa

mbali na zile za mpiga picha mwenyewe.

xi) Haki za nakili

Wapiga picha za magazeti na wasimamizi wa vipindi waheshimu hakinakili na majukumu ya haki za ujirani kuhusiana na kutumia picha zozote nyingine zisizo zao.

xi) Ghiliba

Wapiga picha na wasimamizi wa vipindi vya runinga inapaswa watumie moja kwa moja njia za kupata habari na picha. Kwa kawaida ni kujitambulisha wao wenyewe wakati wanapofanya shughuli zao. Ghiliba inaweza kuhalalishwa tu kwa nyakati nadra kwa maslahi ya umma kwa picha ambayo haiwezi kupatikana kwa njia nyingine yoyote ile. Matumizi ya picha za aina hiyo yaelezwe kama sehemu ya habari.

xii) Picha za kashfa

Picha na alama nyingine zinazoelekea kuwa za kashfa, au zenye nia mbaya, zisichapishwe au kutangazwa.

xiii) Maelezo mafupi chini ya picha

Maelezo ya picha yaandikwe kwa usahihi. Maelezo hayo yawe mafupi yakieleza picha. Lugha yake isiwe ya kibaguzi, kushusha hadhi au kuonyesha watu kwa rangi, imani, jinsia na kabila.

5.5 Vitendo vya kupiga vita rushwa

a) Zawadi na Takrima

Wapiga picha na wasimamizi wa video wakatae tuzo, burudani, zawadi au upendeleo binafsi ambao kwa njia moja au nyingine unashawishi au kuonekana kushawishi kubadilisha maamuzi yao kitaaluma. Zawadi inapotolewa upokeaji wake uarifiwe kwa wakuu wa chombo husika cha habari.

b) Fadhila

Wapiga picha na wasimamizi wa video wasikubali kupokea kitu chochote cha upendeleo ili kuepuka kufika mahali ambapo watalazimika kulipa fadhila hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao. Vivyo hivyo, wasitumie nafasi zao au maarifa waliyopata kutokana na nafasi zao kwa faida binafsi.

c) Malipo ya Habari /Vyanzo

Wasitoe fedha au zawadi kushawishi vyanzo kutoa habari kwani kufanya hivyo ni sawa na kugeuza habari iwe aina ya biashara kitu ambacho hakitakiwi kiwe hivyo.

d.) Kupokea Malipo ya kuchapisha picha

a) Wapiga picha na wasimamizi wa vipindi vya video wasitoe fedha au aina yoyote ya malipo kama kichocheo cha kuchapisha au kutangaza picha au video.

b) Usikubali zawadi, upendeleo, au fidia kutoka kwa wale ambao huenda wakatafuta ushawishi wa kutolewa habari zao.

5.5 Kuingia mahali bila kuruhusiwa

Usiharibu kwa kukanyaga mali ya watu kwa kutembea kwenye eneo lao ili upate muonekano mzuri wa mandhari. Omba kwanza ruhusu kabla ya kuingia eneo lililozuiliwa au lenye mali binafsi na uondoke mara moja unapotakiwa kufaya hivyo.

6.13 Maudhui ya habari za mtandaoni

a) Kwa maudhui ya habari zinazowekwa kwenye mtandao, wapiga picha na wasimamizi wa video watabidi wawe makini kwa kuangalia mara mbili mbili pasipo mashaka maudhui yake ili kuhakiki ukweli, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama habari hizo zimehakikiwa na mtandao.

b) Wataje kikamilifu na wazi wahusika wa habari hizo za mtandaoni.

c) Wanaposhughulikia habari za mtandaoni wafuate sheria na kanuni zinazozingatiwa na tasnia ya habari.

d) Pia itabidi wawajibike kwa matokeo yoyote yale yatakayotokana na vyombo vyao kutumia habari hizo za mtandaoni.

Kanuni za Maadili kwa Waandishi wa Habari

6.0 Waandishi wa Habari

Waandishi wa habari kazi yao ni kukusanya, kuandika na kusambaza habari na taarifa nyingine. Ili kutenda vema shughuli zao za ukusanyaji wa habari kitaaluma na kimaadili, waandishi wa habari watazingatia yafuatayo:

6.1 Kanuni za Maadili

i) Tafuta ukweli wa habari na uripoti

a) Kuwasilisha matukio kwa uhalisia na kikamilifu kama ilivyoelezwa na vyanzo vyote vilivyohusika na suala hilo.

b) Epuka na uongo au kutengeneza habari zinazolenga kudanganya hadhira, kuvuruga ukweli au nia nyingine mbaya.

ii) Uwajibikaji na wajibu

a) Waandishi wa habari watambue jukumu lao kwa jamii na kuwa tayari kufanya ustawi wa jamii kuwa kipaumbele chao badala ya maslahi ya shughuli zao na uhuru binafi.

b) Wataitendea haki habari kama bidhaa ya jamii na siyo ya kuuzwa sokoni. Vivyo hivyo hawatawajibika kwa wanaomiliki vyombo vyao vya habari bali kwa umma kwa jumla ni pamoja na maslahi ya jamii.

c) Watawajibika kwa matokeo yatakayotokana na vitendo vyao vya taaluma au shughuli zinazofanywa au kuchukuliwa kwa hiari na umakini. Chini ya mazingira hayo watafanya shughuli zao kulingana na maadili ya kazi yao.

iii) Kuzuia madhara

a) Watavichukulia vyanzo, watu, waandishi wenzao na wananchi wengine kama binadamu wanaostahili kuheshimiwa

b) Wataonyesha huruma kwa wale ambao huenda wakaathirika na uandshi wao wa habari. Watakuwa makini kwa mambo nyeti hasa wakati wanaposhughulika na watoto na vyanzo au watu wengine wasio na uzoefu.

c) Watakuwa makini wakati wa kutafuta au kutumia mahojiano au picha za wale walioathirika na majanga au huzuni.

iv) Fanyakazi kwa kujitegemea

Mwandishi ataandika habari aliyoipata kwa misingi ya ukweli bila hofu ya kuadhibiwa na bila kushawishiwa na watu binafsi, makundi yenye maslahi au watu wengine wowote wa ndani na nje.

6.2 Kanuni za tunu

i) Haki, Ukweli, Mizania na uadilifu

Tunu za haki, mizania na ukweli zitawaongoza waandishi wa habari katika kazi yao. Wasiwe upande wowote kwenye mambo ya migongano wala wasiminye matumizi ya habari kwa sababu tu ya kuwepo upendeleo kwa mtu au upande mmoja ambao hawaungi mkono. Aidha wasizuie habari kwa amri ya serikali. Wasimlinde mtu awe afisa wa serikali, mmiliki wa chombo cha habari au mtu mwingine maarufu mwenye ushawishi mkubwa. Watu wanaokosolewa katika vyombo vya habari wawe na haki ya kujitetea kujibu mara moja mambo wanayokosolewa. Hata hivyo, haki hiyo isichukuliwe kama silaha bila kuthibitisha uhalali wa madai anayolaumiwa. Waandishi wa habari wajitahidi kuhakikisha kuwa habari za

utata zinaungwa mkono kwa uhakiki wa ushahidi kabla ya kuchapishwa. Kesi ziandikwe bila upendeleo. Katika hatua zote za kesi mwandishi aandike kikamilifu maoni ya pande zote (katika mchakato wa kesi za jinai msimamo wa upande wa mashtaka na msimamo wa upande wa utetezi). Uandishi wa habari za mahakamani lazima uzingatie kanuni kwamba mtu hana hatia mpaka mahakama itakapothibisha na kumtia hatiani mtuhumiwa. Habari inayoweza kuharibu mwenendo wa kesi isichapishwe hadi hukumu itakapotolewa na kesi kufungwa.

ii) Ukweli/usahihi

a) Waandishi waripoti habari ya ukweli ambayo imehakikiwa pasipo mashaka kuhusu ukweli na usahihi wake.

b) Waripoti ukweli katika muktadha upasao kwa kutoa siyo tu ukweli kuhusu suala au mtu bali pia mazingira yanayozunguka muktadha wake.

iii) Uadilifu

Kwa mwandishi kutenda kazi zake kwa uadilifu atapaswa:

a) Kuheshimu na kutii sheria za nchi kwa namna ya mwenendo ambao kibinafsi na umma unakuza imani ya umma, uadilifu wa vyumba vya habari na heshima ya taaluma ya uandishi wa habari.

b) Hataruhusu maslahi ya nje kuweka rehani au kwa namna yoyote ile kuharibu uadilifu wa taaluma, uhuru na uwezo wa vyombo vya habari.

c) Atakataa mwenendo ambao unaweza kuleta taswira ya kutumiwa na watu wenye siri na nia iliyojificha, au kama mtu anayejihusisha

katika rushwa au mtu anayeleta ajenda yake yenye msukomo wa kujifanya kuwa ni sehemu ya kazi ya uandishi wa habari.

d) Wakati unapotafuta habari, mwandishi ni lazima ujitambulishe, kwa kujitaja jina lako na la chombo chako cha habari unachowakilisha na kukiarifu chanzo chako kwamba maneno yake yatachapishwa isipokuwa kama itakuwa vinginevyo.

6.3 Taarifa ya Kanuni/Viwango vya Uhariri

i) Ukweli na Kauli binafsi

Tofautisha kwa uwazi zaidi kati ya mambo ya ukweli, ubahatishaji, maoni na kauli.

ii) Kutokuwa na hatia

Waandishi wa habari watazingatia kanuni ya mahakama ya sheria kwamba katika kesi ya haki kila mtuhumiwa kutokuwa hana hatia hadi mahakama itakapomtia hatiani baada ya upande wa mashtaka na utetezi kutoa hoja zao.

iii) Usiri

Watazingatia usiri kuhusu chanzo cha habari iliyopatikana kwa siri. Pia watakuwa na wajibu wa kuvitaarifa vyanzo vya siri kuhusu masharti ambayo huenda yakawalazimisha wasiheshimu ahadi ya usiri ikiwemo amri ya mahakama.

iv) Habari inayokatazwa

Waandishi wa habari wataheshimu ahadi ya kutochapisha au kutangaza habari inayokatazwa kama walikiahidi chanzo husika.

v) **Wizi wa maandishi na mawazo**

Waandishi wa habari wanatakiwa kuzingatia kanuni kuhusu wizi wa maandishi na mawazo. Wizi wa maandishi na mawazo ni pamoja na

kunakili na kuweka vitu vya watu wengine bila kutaja chanzo na kumtaja mwenye maandishi au mawazo uliyotumia. Wakati anapotumia kazi ya watu wengine mwandishi wa habari atatoa ipasavyo shukrani kwa chanzo cha maneno yaliyokaririwa. Mwandishi hatakariri kutoka chanzo chochote cha habari (vitabu, mtandao, mazungumzo, n.k.) na baadaye kuwasilisha mambo yaliyokaririwa kama yake. Habari ya mtandaoni itumike kama taarifa ya kuifuatlia na isichukuliwe kwa jumla kama habari ya kweli bila kuhakikiwa.

vi) Faragha

Waandishi wa habari watafanya bidii kuelewa mipaka ya maisha ya faragha na umma. Watayaripoti mambo ya umma lakini kamwe siyo kuhusu mambo binafsi ya faragha. Hata hivyo hiyo haitawazuia waandishi wa habari kuripoti kwa haki kuhusu masuala ya mambo binafsi kwa kufichua tabia mbaya ya matendo ya kinyume na jamii, kulinda afya na usalama wa umma na kuzuia unafiki ambapo umma unapotoshwa kuhusu mambo muhimu na mtu masuhuri wa umma au taarifa ya umma au kitendo cha mtu binafsi au taasisi. Waandishi wa habari wanapofanya kazi kwenye maeneo ya hospitali au vituo vingine vya afya wanapaswa kupewa ruhusa kutoka kwa mamlaka zake. Izingatiwe kikanuni kuwa madhara ya dosari za mwili na magonjwa ni siri ya mtu binafsi.

vii) Kutofichuliwa kwa vyanzo

Waandishi wa habari wanawajibika kwa hali na mali kulinda vyanzo vya siri na kuheshimu imani kwa kujua inakubalika kulingana na ajira yao. Hata hivyo mwandishi wa habari atakieleza chanzo chake kwamba ingawa maadili ya taaluma

yanamuhitaji kulinda chanzo, sheria ya nchi inafanya kuwa kosa kama mtu ataitwa mahakamani kutoa ushahidi na kukataa kujibu maswali yaliyoelekezwa kwake au kukataa tu kutaja chanzo cha habari. (Ibara ya 199 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985)

viii) Ubaguzi

Waandishi wa habari wataepuka ubaguzi na uhalifu, taarifa za kashfa au kuonyesha mambo ya ubaguzi wa rangi, imani, jinsia, ukabila, umri, ulemavu, jiografia, mali ya kimwili au hadhi ya jamii. Waandishi wa habari wataepuka kutambua watu kwa ukabila na rangi. Watakuwa makini kwa haki na heshima za watu wenye hali ngumu ya maisha na watoto.

ix) Kashfa

a) Epuka kuchukua na kutoa picha za kashfa za watu binafsi na makundi.

b) Tambua na kufanya kazi kwa kuepuka mambo ya upendeleo ya mtu binafsi katika kazi yako. Wafikirie kwa kipekee watu walioko katika hatari na kuwa na huruma kwa waathirika wa uhalifu na janga.

x) Kashfa

Usitangaze maudhui yoyote au kukuza maudhui ya kashfa na uzushi.

Usifanye kauli isiyo ya moja kwa moja kuhusu mtu au kitu kwa hali ya kushusha hadhi au heshima yake. Wala usibadili maneno kwa njia ambayo wasomaji bado watahusisha maelezo ya stori hiyo na mtu mahsusi.

xi) Uhalifu na Tabia mbaya

a) Usitukuze uhalifu na tabia mbaya katika jamii, hasa kwa kuhusisha vurugu au ukatili.

Usiandike, kuonyesha au kutoa maelezo zaidi ya uhalifu kwa namna ambayo inaweza kushawishi au kuchochea watu kuiga au kufanya majaribio ya matukio hayo. Wahariri waangalie hasa muktadha, athari zinazoweza kutokea na kuelekea kwa usomaji wa habari kama hiyo.

b) Kwa sababu hiyo habari ya aina hiyo isichapishwe au kutangazwa, isipokuwa tu kama imeruhusiwa kisheria na hivyo kwa manufaa ya umma wasitajwe waathirika wa uhalifu na udhalilishaji wa ngono; wala kijana anayeshtakiwa kwa kosa la uhalifu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 na ambaye huko nyuma hajawi kutiwa hatiani na kuwataja bila ridhaa ndugu wa mtu anayeshtakiwa au kutiwa hatiani kutokana na kosa la uhalifu.

xii) Uandikaji wa habari za watoto

Epuka mahojiano ya watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 bila ridhaa ya wazazi wao, walezi au watu wengine wazima wanaohusika nao. Kitu kama hicho kisitokee shuleni bila ruhusa ya mamaka za shule. Uchapishaji wa kitu chochote kuhusu maisha binafsi ya mtoto hakiwezi kuhalalishwa na umaarufu, ubaya au nafasi yake au wazazi. Taarifa zozote hasi kwa watoto zisiwe na majina na anuani zao. Wakati uhalifu unapofanywa na watoto, wakiwa na kesi zinazowasubiri mahakamani majina yao yasichapishwe.

xiii) Waathirika wa Makosa ya Kujamiana

Epuka kuwataja waathirika wa mashambulio ya aibu chini ya makosa ya kujamiana au kutoa maelezo yao zaidi ambako kunaweza kufichua utambulisho wao.

Usitaje majina ya watoto walio na umri wa chini ya miaka 18, wawe waathirika au mashahidi, katika kesi zinazodaiwa kuwa za makosa ya kujamiana. Hata hivyo, watu wazima wanaohusika katika makosa ya kujamiana wanaweza kutajwa lakini isielezwe kama mtu mzima anayetuhumiwa ana uhsusiano wa karibu na mtoto muathirika. Pale wote wanapotambulika basi maneno 'kujamiiana kwa maharimu' yasitajwe.

6.10 Maslahi binafsi na Ushawishi

Waandishi wa habari wasiruhusu maslahi binafsi ya kifamilia yawe na ushawishi katika majukumu yao ya kitaaluma. Wasijiruhusu zawadi na fadhila nyingine zinazoweza kushawishi maoni yao au kujenga taswira kama hiyo, na wasishiriki katika shughuli au mashirika yanayoweza kuweka ukomo wa uhuru wao wa kufikiri na hivyo kuhatarisha uadilifu wa taaluma yao.

a) Wawe huru na vyama, vikundi na shughuli ambazo huenda zikashawishi maamuzi yao kitaaluma, kuweka rehani uadilifu wao na kuhatarisha sifa ya taaluma.

b) Waandishi wa habari wasijihushe na aina yoyote ya ushabiki unaoweza kuathiri msimamao wao wa kutopendelea upande wowote katika habari na kuathiri jinsi atakavyoshughulikia habari husika.

6.5 Vitendo vya kupiga vita rushwa

a) Zawadi na Takrima

Waandishi wa habari wakatae tuzo, burudani, zawadi au upendeleo binafsi ambao kwa njia moja au nyingine unashawishi au kuonekana kushawishi maamuzi yao kitaaluma. Zawadi inapotolewa upokeaji wake uarifiwe kwa wakuu wa chombo husika cha habari.

b) Fadhila

wa habari wasikubali kupokea kitu chochote cha upendeleo ili kuepuka kufika mahali ambapo watahitajika kulipa fadhila hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao. Vivyo hivyo, wasitumie nafasi zao au maarifa waliyopata kutokana na nafasi zao kwa faida binafsi.

c) Malipo ya Habari /Vyanzo

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wasitoe fedha au zawadi kuvutia na kushawishi vyanzo kutoa habari kwani kufanya hivyo ni sawa na kugeuza habari iwe aina ya bidhaa ya kibiashara, kitu ambacho hakitakiwi kiwe hivyo.

d.) Kupokea Malipo ya kutoa Habari

Waandishi wa habari wasipokee fedha au aina yoyoteya malipo kama motisha ya kuchapisha au kutangaza habari.

6.6 Mahusiano yasiyo na Hatia

Waandishi wa habari waepuke kuwataja jamaa wa watu waliotiwa hatiani au kushitakiwa kwa kufanya uhalifu isipokuwa tu kama uhusiano huo unahusika moja kwa moja na habari inayoripotiwa.

6.7 Masuala Yanayohusiana na Imani

Katika masuala yanayohusiana na dini waandishi wa habari hawana budi kuwa na mwelekeo wa usawa, haki na namna inavyoonekana katika hali halisi hata kama taasisi nyingine zote za umma zinahitaji kuchunguzwa, kuhojiwa au kutolewa maoni. Waandishi wa habari hawana budi kutambua umuhimu wa heshima staha waliyonayo waumini kwa viongozi wa dini na wafuasi wao. Kwa hiyo waandishi wa habari watambue umuhimu wa kuwa makini katika mambo ya dini hasa katika jamii yenye imani tofauti.

6.8 Huzuni

Heshimu huzuni ya mtu kwa kuchukua mwelekeo makini na kwa tahadhari katika kuhoji au kuzungumza na waathirika tukio la huzuni. Waandishi wa habari wasiongeze huzuni ya watu ambao tayari wamechanganyikiwa kwa kupoteza wapendwa kwa kushinikiza kutaka wawahoji. Pia waheshimu waliokufa. Kushughulikia matukio ya majanga makubwa kusizidishe maumivu na machungu kwa waathirika.

6.9) Vitendo vya kupiga vita rushwa

a) Zawadi na Takrima

Waandishi wa habari wakatae tuzo, burudani, zawadi au upendeleo binafsi ambao kwa njia moja au nyingine unashawishi au kuonekana kushawishi kubadilisha maamuzi yao kitaaluma. Zawadi inapotolewa upokeaji wake uarifiwe kwa wakuu wa chombo husika cha habari.

b) Fadhila

Waandishi wa habari wasikubali kupokea kitu chochote cha upendeleo ili kuepuka kufika mahali ambapo watahitajika kulipa fadhila hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao. Vivyo hivyo, wasitumie nafasi zao au maarifa waliyopata kutokana na nafasi zao kwa faida binafsi.

c) Malipo ya Habari /Vyanzo

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wasitoe fedha au zawadi kuvutia na kushawishi vyanzo kutoa habari kwani kufanya hivyo ni sawa na kugeuza habari iwe aina bidhaa ya kibiashara kitu ambacho hakitakiwi kiwe hivyo

d.) Kupokea Malipo ya kutoa Habari

Waandishi wa habari wasipokee fedha au aina yoyoteya malipo kama motisha ya kuchapisha au kutangaza habari.

6.10 Uhuru wa Vyombo vya Habari na Wajibu wa Jamii

Waandishi wa habari watatetea uhuru wa vyombo vya habari kwa sababu uhuru huo ni wa watu. Wahakikishe shughuli ya umma inaendeshwa hadharani na lazima kuwa macho dhidi ya wale wanaotumia vyombo vya habari kwa manufaa yao. Katika kueneza habari, waandishi wa habari wabebe mzigo wa kuelewa wajibu wao wa kuelimisha na kuarifu umma kuhusu mambo yanayowaathiri na wajibu wao utakuwa kufuatilia serikali na sehemu nyingine za ushawishi kwa niaba ya wananchi.. Wajibu huo usitumiwe vibaya kwa sababu nyingine zozote. Kataa juhudi zozote za kupotosha habari au udhibiti wake.

6.11 Ghiliba

Wakati wa kukusanya habari, waandishi wa habari wafanye kazi yao kwa uwazi. Kutafuta habari kwa njia za kujificha kunaweza tu kuhalalishwa iwapo habari muhimu kwa jamii haiwezi kupatikana kwa njia nyingine za kawaida.

6.12 Uchochezi

Waandishi wa habari waepuke uchochezi wa kutia mambo chumvi/uongo/upotoshaji na hivyo kushindwa kuandika ukweli. Waandishi wa habari hawana budi kutoa habari ya ukweli na kutoruhusu upotoshaji wa kitu chochote kile.

6.13 Maudhui ya mtandaoni

a) Kwa maudhui ya habari zinazowekwa kwenye mtandao, waandishi wa habari watabidi wawe makini kwa kuangalia mara mbili mbili kuthibitsha pasipo mashaka maudhui yake ili kuhakiki ukweli, muktadha na uhalali wake. Hiyo ifanyike hata kama habari hizo zimehakikiwa na mtandao.

b) Waeleze kwa uwazi kabisa kutumia maudhui ya habari hizo za mtandaoni.

c) Wanaposhughulikia habari za mtandaoni wafuate sheria na kanuni zinazozingatiwa na tasnia ya habari

d) Pia itabidi wawajibike kwa matokeo yoyote yale yatakayotokana na vyombo vyao kutumia habari hizo za mtandaoni.

Miongozo kwa Wamiliki wa Vyombo vya Habari na Wachapishaji

7.0 Wamiliki wa Vyombo vya Habari/Wachapishaji

Hawa ni watu binafsi au kikundi cha watu, taasisi au shirika linalomiliki gazeti, kituo cha redio, kituo cha runinga au chapisho la mtandaoni. Wakati mwingine mmiliki wa chombo cha habari/mchapishaji huwa ni mtu binafsi anayeongoza kampuni ya uchapishaji. Kwa wao ili kudumisha viwango vya juu vya taaluma na uadilifu ni lazima wazingatie yafuatayo:

7.0 Uhuru

Dumisha mfumo, ulio huru kwa mwandishi na mhariri. Hata hivyo hawataingilia kazi ya uhariri ikiwa pamoja na kuangalia na kuhakiki ukweli katika makala zote na mambo mengine yaliyochapishwa au kutangazwa.

7.1 Ushindani

Epuka mashindano ya masharti na ushindani uwe wazi kwa wote.

7.2 Shinikizo au Ushawishi

Epuka ukandamiza au upotoshaji wa habari ambayo umma unayo haki ya kujua kwa sababu ya shinikizo au ushawishi usiostahili kutokana na maslahi ya kibiashara, kisiasa, kijamii, kiuchumi au dini.

7.3 Malipo ya Habari na Mauzo

Epuka kuchapisha au kukandamiza ripoti za uhariri au kuacha au kubdili ukweli muhimu katika ripoti hiyo ili kupata malipo ya fedha au zawadi au tuzo ya aina yoyote ile. Hata hivyo kanuni hii ya maadili haitatumika

kwa matangazo au tahariri ya makala ya tangazo.

7.4 Uchunguzi

Wamiliki wa vyombo vya habari wakubali uchunguzi wa mambo yao wenyewe. Uchunguzi huo sio wa kiserikali bali chini ya taratibu uliowekwa na vyombo vyenyewe vya habari, kama Baraza la Habari Tanzania(MCT), linalosimamia uwajibikaji wa kidemokrasia wa vyombo vya habari kwa umma.

7.5 Migongano ya Maslahi

a) Wamiliki wa vyombo vya habari wasitumie vyama, nafasi na shughuli zao kushawishi vyombo vyao vya habari kukiuka madili na viwango vya weledi.

b) Watawaachia wanataaluma wa habari kufanya maamuzi ya mwisho kuhusu kazi za uhariri. Katika njia zote, uandishi wa habari au makala lazima uwe kwa msingi wa kile mhariri anachoamini kuwa ni kwa maslahi ya wasomaji/watazamaji/wasikilizaji na siyo kwa nia na maslahi ya wamiliki wa vyombo vya habari au wachapishaji.

7.6 Shinikizo au ushawishi

Uwe huru na majukumu mengine mbali na haki ya umma kujua pamoja ustawi wa jamii. Kwa maneno mengine, wakuu wa vyombo vya habari na wahariri hawatakandamiza au kupotosha habari ambayo umma una haki kujua kwa sababu tu ya shinikizo kutokana na maslahi ya kisiasa, kibiashara au kijamii.

7.7 Ushabiki

Wamiliki wa vyombo vya habari wasihusishe vyombo vyao katika aina yoyote ya ushabiki ambao huenda ukaweza kuvilazimisha visisimame imara kulinda na kutetea viwango na maadili yao kitaaluma.

7.8 Uwezo Kitaaluma

Wamiliki wa vyombo vya habari watawezesha wafanyakazi wao kwa kuimarisha uwezo wao kitaaluma kupitia mafunzo na kuendeleza zaidi stadi za kazi. Zaidi ya hayo, wamiliki wa vyombo vya habari wahakikishe kuwa waandishi na wafanyakazi wengine wanaongezewa utaalamu na ubunifu mpya katika tasnia ya mawasiliano.

7.9 Mishahara na Marupuru

a) Wamiliki wa vyombo vya habari wawalipe watumishi wao kwa mujibu wa sifa zao kitaaluma na utendaji wa kazi.

b) Wawe na muundo wa utumishi unaoelezea wazi masuala kuhusu marupurupu na motisha nyingine.

7.10 Shuruti na Vitisho

a) Wamiliki wa vyombo vya habari/Wachapishaji wapendekeze mambo na kutoa hisia zao kwa mameneja bila kutumia nguvu na vitisho. Aidha watumie zisizo na vurugu kumaliza kutoelewanai.

b) Wamiliki wa vyombo vya habari/wachapishaji wawalinde wanahabari wao wanaotishiwa kushambuliwa, kuharibiwa zana zao za kazi na ofisi hadi vitisho hivyo vitakapomalizika.

7.11 Uwajibikaji kwa jamii

i) Wazingatie wajibu wao kwa jamii, unaotaka vyombo vya habari kuweka msisitizo zaidi katika ukuzaji wa ustawi wa jamii badala ya maslahi tu ya kibiashara.

ii) Wasiingilie kwa sababu yoyote vyombo vyao katika kufuatilia serikali na vituo vingine vya ushawishi kwa niaba ya umma.

7.12 Wajibu na Uwajibika

Wamiliki wa vyombo vya habari/Wachapishaji watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kutoa kipambaule kwa ustawi wa jamii kwa gharama ya maslahi ya shughuli zao na uhuru binafsi.

7.13 Kushughulikia maudhui mapya ya vyombo vya habari

Watawajibika kwa matokeo yoyote yatakayotokana na habari za mitandanoni zitakazotumiwa na vyombo vyao.

MAREJEO :
Tara K. Harper (2004), On Publishers and Getting Published, Retrieved 28 May 2010.
Randall, D. (2000), The Universal Journalist, Sterling Virginia: Pluto Press.
Mackay, A. (2004), The Practice of Advertising, London: Butterworth-Heinemann.
Vaughn, S. L. (ed) (2008), Encyclopedia of American Journalism, New York: Routledge.
The Chief Communications Officer: A Survey of Fortune 200 Companies, Korn/Ferry Institute, April 2009
Vaughn, S. L. (ed) (2008), Encyclopedia of American Journalism, New York: Routledge.
Mamishev, A. and Williams, S. (2009), Technical Writing for Teams: The STREAM Tools Handbook, Institute of Electrical and Electronics Engineers, John Wiley & Sons. Inc., Hoboken, p.128
Vaughn, S. L. (ed) (2008), Encyclopedia of American Journalism, New York: Routledge.
Schivinski, B and Dąbrowski, D. (2014), The Effect of Social-Media Communication on Consumer Perceptions of Brands, Journal of Marketing Communications: 2–19.
Manovich, L. (2003), New Media from Borges to HTML, In: Noah Wardrip-Fruin& Nick Montfort (eds), The New Media Reader, Cambridge, Massachusetts, 13-25.
Hall, J (n.d), Online Journalism: A Critical Primer, London: Pluto Press